Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa; na kwa yakini Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kuwasaidia.
Waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu wanasema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu. Na kama Mwenyezi Mungu Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu hutajwa kwa wingi. ... 22:40-41.

JUZU 74 No. 177 | DHULQA'DAH/HIJJA 1434AH | SEPTEMBA/OKTOBA 2013 | IKHA/TABOOK 1392 HS | BEI TSH. 500/=

Jalsa Salana ya 44 Tanzania yazidi kung'aa

Watu wapatao 3,000 wahudhuria Ukumbi mpya wa akinamama waanza kutumika

Na Mwandishi wetu

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu Jalsa Salana (mkutano wa Mwaka) ya 44 ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania imefanyika kwa mfanikio makubwa. Alhmadulillah.

Jalsa hiyo imefanyika tarehe 27 – 29 Septemba, 2013 huko Kitonga, Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam. Waumini wapatao 3000 kutoka ndani na nje ya Tanzania walihudhuria mkutano huo. Wageni waliohudhuria ni kutoka Uingereza, Uganda, Burundi na Malawi. Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Uganda Sheikh Afzaal Ahmad Rauf alikuwa ni miongoni mwa wageni saba waliotoka nchini humo.

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu mkutano wa mwaka ulikuwa wa mafanikio maalum kwani kumbi zote mbili za wanawake na wanaume ambazo ni sehemu ya ukumbi wa maadhimisho ya miaka 100 ya Khilafat zilikuwa zimejengwa kwa kiwango cha kuweza kutumika. Kiini cha Jalsa Salana ya mwaka huu kilikuwa ni: **'Mafundisho ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. ndio suluhisho la kuleta amani ya dunia.'**



Sehemu ya wahuhduriaji kwenye Jalsa salana ya mwaka 2013 wakisiliza kwa makini hotuba ya ufunguzi iliyotolewa na Amir na Mbashiri

Akifungua Jalsa Salana hiyo, Amir na Mbashiri wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib aliwakumbusha wahudhuriaji wa Jalsa hiyo kwamba ni lazima muda wote wakumbuke juu ya lengo la kuanzishwa kwa Jalsa Salana pamoja na kujitahidi kulifikia lengo hilo.

Akilitaja lengo la kuanzishwa

Endelea uk. 2

Ndoto 3 tukufu za Mtume Muhammad s.aw

Ustadhi ***A .R. Mikila – Morogoro***

Kutoka toleo lililopita

NDOTO ZA MTUME MUHAMMAD (SAW).

Ndoto za Mtume Muhammad (saw) zilikuwa za daraja la juu na za ubora mkubwa sana. Yeye alitumwa kwa ajili ya watu wote wa dunia hii, wa zama zake, wa zama hizi na zama zote zijazo.

Hii ndivyo kauli ya Qurani tukufu:-

"Sema: Enyi watu, hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyote,.. " (Kur 7:159)

Hapo mwazoni nilisema kwamba, ndoto ni onyesho la mambo yanayo patikana wakati mtu yumo usingizini amelala. Mambo yote yale atakayo yaona usingizini, hata kama yatahusu mambo aliyo yazoea, lakini yatakuwa yamepambwa na alama maalum za viashiria vya ndoto, yatayokuwa kinyume na uhalisia wake. Kwa sababu hiyo, ndoto huhitaji tafsiri ili kuzifahamu maana zake na tabiri zilizo jificha.

Tuchukulie kwa mfano, *mtu amejiona katika ndoto, ametembelewa na rafiki yake aliye fariki zamani. Rafiki yule akomba kwake mkopo wa fedha kukidhi shida fulani. Na yeye akampa mkopo ule na kuandikishiana naye hati ya deni. Lakini mle ndotoni, huyu mkopeshaji akajiona anashangaa kuona ana andikishianaje deni na mtu aliye kwisha kufa?*

Hivi itaingia akilini kwamba, mkopeshaji huyu wa ndotoni, akiamka usingizini asubuhi, aende kwa ndugu na jamaa wa marehemu kudai deni lile? Mbona itashangaza sana, atakapo sema kuwa usiku wa jana, marehemu rafiki yake alikuja kwake kuomba mkopo wa pesa kiasi fulani, na kwamba yeye alimkopesha pesa hizo. Kwa hiyo sasa, nduguze wanapaswa wamlipie deni lile. Kila mwenye akili timamu atamuona mtu huyu ni punguwani au Juha. Iweje deni la ndotoni liwe ni deni halisi? Hata kama mkopeshaji huyu, ang'ng'nie kwamba ile haikuwa ndoto, bali ni kweli marehemu mwenyewe alikuja kuomba mkopo. Lakini wasikilizaji wake watamjulisha kuwa walio

Endelea uk. 4

Alhamdulillah, tumefanya Hija

Mwl. Hassan Mrope na Amir Abedi Kaluta

Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwingi wa ukarimu.

Tulifanya ibada ya Hija aina ya Tamatui ambayo inaanza kwa kufanya Umra kisha Hija. Katika Hija hii ya aina ya Tamattui unapomaliza Umra unalazimika kuivua Hiramu kisha kuiavaa tena Hiramu kwa ajili ya Hija. Kuna Hija za aina mbili zingine zinazoitwa Ifraad na Qiraan.

TULIVYOFANYA IBADA YA UMRA

1. Tulihirimia kwenve Miikati ya Abaar Alii Jumanne asubuhi tarehe 8/10/2013 (tarehe 3 Dhulhijja)
2. Kisha tulitufu Kaaba mara saba usiku wa Jumanne tarehe 8/10/2013 (tarehe 4 Dhulhijja)
3. Kisha tukasali rakaa mbili nyuma ya Makamu Ibrahimu.
4. Kisha tulisai baina ya Safwa na Marwa mara saba.
5. Kisha tulipunguza nywele.

Hapo tukawa tumemaliza ibada ya Umra, tukarudi hotelini na kavua Hiramu. Hiyo ilikuwa ni asubuhi ya jumatano tarehe 9/10/2013 (tarehe 4 Dhulhijja)

TULIVYOFANYA IBADA YA HIJA

1. Tulihirimia hotelini kwetu mjini Makka kabla ya alfajiri Jumapili tarehe 13/10/2013 (tarehe 8 Dhulhijja)

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

NJIA PANDA

Kila taifa hapa duniani hapana shaka lipo safarini. Inaonesha ni safari ndefu na ngumu, na katika safari hiyo kila taifa hufika njia panda, mahali alipofika Robert Frost na kushangaa kwamba njia mbili ziliingia msituni na kwa sababu ni mtu mmoja asingeweza kutembea njia hizo mbili kwa pamoja. Ni kweli binadamu hawezi kutembea njia mbili mara moja. Tunahitajiwa kufanya uamuzi kwani kusimama bila kufanya uamuzi ni dalili ya mtu mwoga na mwoga hufa mara nyingi kabla ya kifo.

Tulipofika sisi Watanzania panatukumbusha kizungumkuti alichokumbana nacho Hamlet cha kuendelea kuishi au kutoa maisha yake. Kama taifa hatuna njia ila kuendelea kupumua, lakini kuendelea kwetu kupumua lazima tufanye uamuzi kuhusu katiba. Yaani makubaliano baina ya watawala na wataliwa.

Kuna uhodari na mbwembwe nyingi zimejitokeza katika mchakato mzima unaohusika na katiba. Uchambuzi wa kina umefanyika. Tume imeundwa, imetembea kadri ilivyowezeshwa. Mwisho wa safari hiyo ndefu tume ikatoa iliyoyakusanya. Ningeshangaa tena ningeshangaa mno, ningeambiwa kuwa waliowakilisha yamekamilika. Hilo haliwezekani. Kutofautiana ni rehema na baraka. Wapo wanaosema tuwe na serikali tatu. Wapo wanaosisitiza wawe na Dola, fedha na kiti kwenye umoja wa mataifa. Wapo wanaotaka Tanganyika yao, wapo wanaotaka mfumo wa muungano tulio nao uendelee. Sote tuna nia nzuri. Sote ni watanzania. Sote ni wazalendo. Sote tuna uchungu na taifa hili. Hakuna mwenye haki ya kujidai kwamba yeye anaipenda Tanzania kuliko mwingine. Kwa kipimo gani? Kwa kigezo gani? Si dhambi asilani watu kutofautiana kifikra.

Hoja nyingi zimejengwa kwamba watu wanatafuta maslahi yao binafsi. Wapo wanaosema wale wanaofaa kuwa viongozi hawapendi kuongoza na wale wenye pupa ya kuwa viongozi

sio tu kuwa hawafai, bali hawawezi.

Yote hayo ni m azito na huenda yakawa na ukweli. Tatizo letu kama binadamu ni kwamba sisi ni dhaifu, tena ni dhaihfu sana. Hatuna elimu ya ghaibu wala hatujui yatakayotokea dakika mbili zilizo mbele yetu. Kwa kutambua udhaifu Allah Ametupa silaha moja muhimu nayo ni maombi. Kumuomba Allah ili Atuongoze katika njia iliyonyooka na tuepukane na miba yote iliyo njiani.

Tizama mwanadamu alivyo dhaifu, hata namna ya kuomba anafundishwa. Yeye peke yake hawezi na huo ndio umekuwa utamaduni wa taifa letu. Chama cha TANU kilicholeta ukombozi wa taifa letu kilikuwa kikianza vikao vyake kwa dua. Siku ya Uhuru tarehe 09/12/1961 waliitwa viongozi wa dini ili waendeshe maombi. Wimbo wetu wa taifa ukiusikiliza kwa makini sana ni maombi matupu. Bunge letu linafunguliwa kwa maombi na kufungwa kwa maombi.

Ni hoja hafifu tena hafifu sana kukataa hoja kwa sababu inatoka kwa fulani. Huenda siku hiyo akawa na hoja madhubuti. Kinachotakiwa ni uzito na uzuri wa hoja bila kujali au kutazama urefu au ufupi wa mtoa hoja. Hekima kama yalivyo maua huota m ahali popote pale. Mtukufu Mtume Muhammad (saw) anasema; 'Hekima ni mali ya Muaminio iliyopotea na popote utakapoikuta uichukue'. Kung'ang'ania kuwa hii ni hoja ya watu fulani hivyo tuipinge kwa nguvu zetu zote na tusiwape ushindi au ujiko watu fulani ni dalili tosha za kupoteza muelekeo. Tutulie tusikilize hoja. Kama ina mantiki ni mali yetu Watanzania tuitumie asaa ikatusaidia katika ujenzi wa mustakabali wa taifa letu.

Sasa kuliko wakati wowote ule, tunatakiwa tufanye maombi ili Allah Atuongoze tupate katiba itakayokidhi haja ya ujenzi wa taifa lenye uadilifu, huruma na mapenzi. Mshairi John Milton anasema vitu vingi vinaletwa na maombi kuliko hata tunavyoweza kufikiri. Huu ni wakati wa kufanya maombi ili Allah Atuongoze tupate makubaliano ambayo yataendeleza lakabu yetu ya kuwa kisiwa cha amani. Kila mwenye uchungu na taifa letu anatakiwa aanguke kwenye kizingiti cha Allah ili aweze kulivusha jahazi la taifa salama salimin na tuendelee kutekeleza shabaha ya kuumbwa kwetu ambayo ni kumwabudu Allah na kutimiza wajibu wetu kwa viumbe wake. Mungu ibariki Tanzania.

Alhamdulillah, tumefanya Hija

Kutoka uk. 1

2. Kisha tulienda Mina na kufika hapo kabla ya adhuhuri siku hiyo hiyo ya jumapili tarehe 13/10/2013 (tarehe 8 Dhulhijja). Tulisali hapo Mina sala ya safari wakati wa adhuhuri, wakati wa alasiri, wakati wa magharibi, wakati wa isha na kesho yake, Jumatatu tarehe 14/10/2013 (tarehe 9 Dhulhijja), sala ya alfajiri. Kila sala kwa wakati wake.
3. Kisha tukaondoka kuelekea Arafat na kufika hapo asubuhi siku hiyo hiyo ya Jumatatu tarehe 14/10/2013 (tarehe 9 Dhulhijja). Tulisali sala ya safari kwa kuchanganya adhuhuri na alasiri wakati wa adhuhuri. Kisha tukaanza Istighfaar na Dua kuanzia adhuhuri hadi magharibi kwenve bonde hilo la Arafat.
4. Kisha tulielekea Muzdalifa wakati wa magharibi siku hiyo hiyo ya Jumatatu tarehe 14/10/2013 (tarehe 10 Dhulhijja). Tulisali sala ya safari hapo Muzdalifa kwa kuchanganya sala ya magharibi na Isha wakati wa Isha. Tulikesha hapo Muzdalifa kwa kufanya Dhikirillah hadi alfajiri Jumanne tarehe 15/10/2013 (tarehe 10 Dhulhijja). Tukasali hapo sala ya alfajiri.
5. Kisha tulirudi Mina asubuhi Jumanne tarehe 15/10/2013 (tarehe 10 Dhulhijja) na kufika hapo asubuhi hiyo hiyo. Tulisali sala ya adhuhuri na ilipofika Alasiri tulisali sala ya safari ya alasiri.
6. Kisha tulielekea Jamarat kurembea vijiwe saba kwenye Jamratil al Akaba na kurudi kwenye hema letu.
7. Baada ya viongozi wetu kutuhakikishia kwamba kuchinja mnyama tayari kumeisha fanyika basi tukanyoa kipara na kuvua Hiramu na kubakia hapo Minna tukiendelea na DhikirLlah.
8. Jumatano alasiri Tarehe 16/10/2013 (tarehe 11 Dhulhijja) tulienda jamarat kurembea vijiwe 21, saba kwenye nguzo ya kwanza, saba kwenye nguzo ya kati na saba kwenye nguzo ya tatu ambayo ndiyo Jamratil ala Akaba. Kisha tulirudi kwenye hema letu kuendelea na dhikriLlah.
9. Alhamisi tarehe 17/10/2013 (tarehe 12 Dhulhijja) wakati wa Alasiri tulienda tena Jamarat kuremebea vijiwe 21 kama tulivyofanya jana yake. Kisha tulirudi kwenye hema letu kuendelea na dhikrLlah.
10. ljumaa tarehe 18/10/2013 (tarehe 13 Dhulhijja) baada ya sala ya adhuhuri tulienda tena Jamarat na kuremebea vijiwe 21 kama tulivyofanya kila siku katika siku mbili zilizopita kisha tuliondoka Mina na kurejea hotelni kwetu mjini Makka. Siku hiyo hatukusali sala ya Ijumaa bali sala ya safari ya kawaida wakati wa adhuhuri bila ya kuchanganya na Alasiri.
11. Usiku wa kuamkia Jumamosi tarehe 19/10/2013 (tarehe 14 Dhulhijja) tulienda kutufu Kaaba mara saba. Hii inaitwa Tawafu Ifadha
12. Kisha tulisali rakaa mbili nyuma ya Makamu Ibrahim.
13. Kisha tulifanya Sai baina Safwa na Marwa mara saba. Hapo tukawa tumemaliza ibada ya Hijja.
14. Usiku wa kuamkia siku ya kuondoka Makka kurudi nyumbani tulitufu tena Kaaba mara saba. Hii inaitwa Tawafu Nidaa (tawafu ya kuaga). Tawafu hii haifuatiwi na kusali rakaa mbili nyuma ya Makamu Ibrahimu wala kusai.

Jalsa Salana ya 44 Tanzania

Kutoka uk. 1

kwa Jalsa Salana, Sheikh Tahir alisema kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. alianzisha Jalsa Salana kwa amri ya Mwenyezi Mungu ili Wanajumuiya kwa pamoja wapate nafasi ya kusikiliza hotuba za kielimu na zenye mafunzo ya kukuza maendeleo yao ya kiroho ili waweze kukuza Uchamungu. Hivyo alisisitiza kwamba kukuza uchuamungu ndio lengo kuu la Jalsa Salana na wakati wa Jalsa na hata baadae katika kipindi cha mwaka mzima tuhakikishe kwamba tunalizingatia jambo hili.

Mgeni rasmi katika Jalsa Salana ya mwaka huu alikuwa ni Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ingawaje kutokana na mazingira yaliyompelekea ashindwe kufika alimteua Bw. Agostino Shio ili amwakilishe kwenye mkutano huo.

Akiongea kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Bw. Shio alisema: "Watanzania ni watu tuliozoea katika kuishi pamoja na kuleta utangamano na ushirikiano baina ya watu wa makundi mbalimbali yawe ya dini, siasa, makabila n.k. Lakini siku za karibuni tumeanza kuona dalili zote za uvunjifu wa amani katika jamii zinazosababishwa na makundi mbalimbali. Ukichunguza sana utaona ya kwamba wapo watu wachache wenye uroho na ubinafsi hawaitakii nchi yetu mema na hivyo kuanza kuipaka matope ambayo si asili yake. Kwa pamoja tuna wajibu wa kuwakemea na kuwadhibiti watu hawa.

Pia alisema: "Dini na viongozi wa dini wanayo dhima katika kujenga jamii ambayo itakuwa salama, yenye upendo ambayo kila mtu ataifurahia kuishi. Kwa kufanya hivi kila mmoja atakuwa amepewa fursa ya kumshukuru Mungu aliye muumba wetu.

Uvunjifu wa amani ndani ya nchi hii ni miongoni mwa matukio yanayochukuliwa kuwa ni uhalifu. Ukweli ni kwamba atakayefanya uhalifu akiwa ni mtanzania au si mtanzania, ukiondoa wale wasioamini kuwepo kwa Mungu – ambao ni wachache katika nchi yetu - atakuwa anatokana na dini au dhehebu fulani la dini. Aidha waumini wetu ndio hao hao ambao baadhi yao wanakuwa ndiyo wahalifu na kusababisha uvunjifu wa amani katika jamii. Viongozi wa dini wanao wajibu mkubwa wa kuisaidia serikali katika kutoa mahubiri na mafundisho yenye kuwajenga waumini wao katika kuienzi amani.

Mafundisho ya kuigawa nchi kamwe hayawezi kutusaidia. Hivyo muwaeleze waumini wenu uhalisia wa mambo wa kuona thamani na kuitunza amani tuliyonayo leo. Natoa wito kwako na uongozi wako, pamoja na viongozi wa dini na imani zingine kwamba msiwaogope waumini wenu kuwaeleza ukweli huu kwa kuchelea vyeo vyao, elimu zao nafasi zao za kisiasa, au vipato vyao vikubwa ambavyo wanachangia sadaka kwa wingi kwenye nyumba za ibada. Kwani amani itakapoondoka hayo yote yatatoweka.

Bw. Shio alimalizia hotuba yake kwa kusema: Nafahamu ya kwamba dini yenu ya kiislam inasema kuipenda nchi ni sehemu ya imani, Mungu Ametufanya kuwa watanzania hivyo tunawajibika kuipenda nchi yetu kwa moyo wetu wote. Tutumie kila fursa iliyopo katika kuijenga nchi yetu na tunawajibika kuinusuru nchi yetu isije ikaingia katika dimbwi baya la kukosa amani.

Wageni wengine waliohudhuria Jalsa hiyo alikuwa ni Bw.

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Jalsa Salana ya 44 Tanzania

Kutoka uk. 2

Mohammed Swai aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Iringa. Wengine ni Bw. Ali Mohammed aliyemwakilisha Diwani wa Mwananyamala na Bi Lai Ali Ninga aliyemwakilisha Mbunge wa Jimbo la Ukonga.
Aidha Mh. Fredirick Sumaye, Waziri Mkuu mstaafu na Diwani wa Kata ya Msongola Bibi Magombeka walituma salamu zilizosomwa kwenye mkutano huo.

Mkutano huo uliripotiwa vya kutosha kwenye vyombo kadhaa vya habari, kwani hata kabla ya tarehe ya Jalsa mnamo tarehe 24 Septemba 2013 ulifanyika mkutano na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo huko ofisini kwa Amir Jamaat Makao Makuu Mnazi Mmoja Dar es Salaam. Vyombo vilivyotoa taarifa za mkutno huo ni pamoja na: The Guardian, Majira. Mtanzania,, Uhuru Nipashe, TBC1, Dailynews,, Habarileo, The Citizen, BBC radio Swahili services na Channel Ten.

Aidha, sambamba na kufanyika kwa Jalsa Salana, Wanajumuiya walichangia damu kiasi cha Paint 500 katikamfuko wa Taifa wa damu salama.

Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. alituma salamu maalum za kuitakia kheri Jalsa Salana hiyo.



Kutoka kushoto: Sheikh Afzal Ahmad Amir na Mbashiri Mkuu wa Uganda, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania Bw. Augostino Shio Mgeni rasmi aliyemwakilisha Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani na Bw. Seif Hassna Nakuchima Katibu Mkuu.

Salamu za Khalifa Mtukufu a.t.b.a. kwenye Jalsa Salana Tz 2013

بسم الله الرحمن الرحيم

Mirza Masroor Ahmad
KHALIFATUL MASIH V
Wapendwa Wanajumuiya wa
Ahmadiyya Jamaat Tanzania
Assalaam alaikum warahmatullah wabarakaatuh.

Nimefurahishwa sana kwamba mnafanya Jalsa Salana yenu kuanzia tarehe 27, 28 na 29 Septemba 2013. Allah na Aibariki Jalsa Salana yenu kwa mafanikio makubwa na manufaa makubwa yatokanayo na rehema kuu za kiroho zilizomo katika kikao hiki kilichobarikiwa wayapate washiriki wote.

Kumbukeni, katika kipindi cha Jalsa, msijiingize katika maongezi ya kipuuzi, Mbakie wakati wote katika hali ya maombi na Istighfar. Sikilizeni kwa makini hotuba zote za wataalamu wa Jamaat, na hivyo muongeze elimu na ufahamu wenu wa mafundisho ya Islam na mpate kila namna ya baraka zitakazowawezesha kuwa Waislamu Waahmadiyya bora zaidi.

Kama Waislamu Waahmadiyya mnatazamiwa kuweka mifano ya hali ya juu kabisa ya wema, uaminifu, kujiheshimu na muhimu zaidi – uchamungu na utawa. Yawapasa kufuata amri za Mwenyezi Mungu na msizichukulie kiwepesi. Badala yake yawapasa kuheshimu kila moja ya amri Zake na kuthibitisha heshima hiyo kwa matendo yenu. Msikubali kuruhusu kitendo chenu chochote kuwa pungufu ya viwango vya juu vilivyowekwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Kuhusiana na jambo hili Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) ametuhimiza kwa kusema:

"Lengo la kujiunga na Jumuiya ni kujenga mahusiano na mimi kama yale ya kiufuasi ili kwamba wafikie kiwango cha hali ya juu cha uchaji Mungu na utawa. Utendaji maovu wowote au uasi usipate kuwakaribia. Wanatakiwa wasali sala tano za kila siku bila kukosa na kwa jamaa, na wasiseme uongo au kumuumiza yeyote kwa ndimi zao. Hawapaswi kuwemo katika upotevu wowote. Na hawatakiwi kuruhusu hata wazo la uasi, ukosefu au kuvuka mipaka lipite katika fikra zao. Wanapaswa kuchukia kila aina ya dhambi, uchokozi, kauli na matendo yasiyopendeza na matamanio ya kinafsi na tabia mbaya zote. Wanatakiwa kuwa na mioyo iliyotakasika, wasimdhuru mtu na wawe watumishi wapole wa Allah mwenye Enzi na kusiwepo kimelea chochote cha sumu kinachoshawishi katika nafsi zao." ."[Essence of Islam, Vol IV, pp 349-350].

Kumbukeni vile vile, mkiwa Waislamu Waahmadiyya, wajibu wenu hauhusu nchi yenu tu, bali mnao wajibu kwa wanadamu wote. Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

"Muwe wema na warehemevu kwa wanadamu kwa kuwa wote ni viumbe Wake. Msiwakandamize kwa ndimi zenu, mikono yenu au kwa njia nyingine yoyote ile. Daima mjishughulishe kwa manufaa ya wanadamu. Kamwe msijinasibu kwa majivuno juu ya wengine, hata wale walioko chini yenu. Msitumie lugha dhalilishi juu ya mtu yeyote, hata mtu huyo akiwatukaneni. Kuweni wapole wa moyo, wema, laini na wasamehevu, wenye huruma kwa kila mtu na kuwatakia heri ili mpate kukubaliwa …. Kama muwe wakubwa kuweni wenye huruma kwa wadogo, na msiwadharau. Kama mkiwa wajuzi na wenye maarifa bora ya kielimu, watumikieni wasio na elimu kwa meneno ya busara, kamwe msitake kuwaumbua kwa kukosa kwao elimu kwa kujaribu kujionyesha katika elimu zenu. Kama mkiwa matajiri badala ya kuwatendea kwa majidai, na bezo la kujiona, yawapasa kuwatumikia walio maskini" [Kashti- Nuh: Roohani Khaza'in vol 19 PP- 11-12]

Anasema pia:

"Narudia kwamba wale ambao wanawanufaisha wanadamu na wanakamilika katika imani, kwa uaminifu na uadilifu, bila shaka yoyote wanaokolewa. Kwa hiyo mwapaswa kujitahidi kukuza sifa hizi ndani yenu." " [Malfoozal, New Ed. Vol 4 p.184].

Vile vile nawakumbusheni juu ya wajibu wenu katika kufanya mahubiri ambayo ni jambo la msingi katika maisha ya kila Muahmadiyya. Furaha ya kweli yaweza tu kupatikana kwa kueneza ujumbe mwanana wa Mtume Mtukufu (s.a.w.) kila pembe ya nchi yenu, na kila pembe ya ardhi; kwa kufikisha ujumbe huu mzuri kwa kila mmoja wa watu waliomo duniani na kwa kumsalia (Daruud) Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w).

Nimekuwa pia nikieleza umuhimu wa maombi katika nyingi ya hotuba zangu na kwamba wanajumuiya wote wafanye maombi maalum kwa sababu ya mateso makali yaumizayo ambayo Waahmadiyya wanayapata katika baadhi ya nchi duniani. Kuhusiana na maombi Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) alisema:

"Katika kipindi kati ya maombi na kupokelewa kwake mtu mara nyingi huwekwa kwenye mtihani baada ya mtihani, baadhi ya hiyo ikiwa ni ya kuvunja mgongo. Muombaji asiyekata tamaa na mwenye asili njema husikia manukato ya msaada wa Mola wake katika mitihani hii na mataabiko, na akili yake inamuambia kwamba haya yote yatafuatiwa na msaada. Sifa moja ya mitihani hii ni kwamba inaimarisha hamu ya kufanya maombi. Kadiri taabu ya muombaji inavyokuwa kubwa, ndivyo kadri roho yake itakavyoyeyuka. Hali hii ni moja ya mahitajio ya kukubaliwa kwa maombi. Kwa hivyo mtu asikate tamaa na asimfikirie vibaya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya haraka na kukosa subira. Mtu asifikiri kamwe kwamba maombi yake hayakupokelewa au kwamba hayatapokelewa. Fikra kama hii ni kukinzana na sifa ya Mungu ya kupokea maombi" [Malfoozat vol IV Essence of Islam. vol II, p. 222].

Tumempokea Imam wa zama na kwa bahati mbaya tunaonewa na wakandamizaji kwa sababu tumemwamini yule aliyetumwa na Mungu katika zama hizi.

Kwa hakika kabisa tunayavumilia yote haya kwa ajili ya Mungu, kwa hiyo kwa hakika kabisa, Atayajibu maombi yetu, kama ambavyo kwa hakika anayasikiliza. Maendeleo ya Jamaat Ahmadiyya ni mfano hai wa jambo hili. Ingawa mipango ya adui imejaa hatari nyingi dhidi ya Jamaat, ni rehema ya Mungu kwamba ili kuimarisha imani zetu, Anahafifisha njama zao mbaya katika matukio mengi sana.

Vile vile nakushaurini mbakie mmeshikamana na taasisi iliyobarikiwa ya Ukhalifa. Zisikilizeni bila kukosa hotuba zangu na wahimizeni wanajumuiya wote watoto kwa wakubwa kufanya hivyo. Kama hamuwezi kuzisikiliza hotuba zangu moja kwa moja, basi sikilizeni rekodi zake, lakini ni muhimu kwa kila mwanajumuiya apate ujumbe wa leo na miongozo ya Khalifatul Masih. Leo hii kazi ya kuihuisha Islam inaweza tu kufanikiwa kwa kushikamana na mfumo wa Khilafat. Kwa hiyo mwapaswa siku zote kujitahidi kuienzi taasisi hii yenye baraka na kuhakikisha kwamba vizazi vyenu vijavyo siku zote vinabakia ndani ya muongozo uliobarikiwa na ulinzi wa Khilafat Ahmadiyya.

Namuomba Mungu kuwa aongeze mapenzi baina yetu, utulivu na kuhurumiana na tuwe Jumuiya ile ambayo Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) alikusudia kuanzisha duniani, tujitoe kwa dhati katika kuwatumikia wanadamu.

Allah na Aibariki Jalsa yenu kwa kila mafanikio na Ajaalie nyinyi nyote mjawe na roho mpya, wema na ucha Mungu, ili muweze kwenda mbele na kuitumikia Islam na wanadamu, kwa nguvu mpya ya kiroho na hamu.

Allah na Awabariki wanajumuiya wote na watu wazuri wa Tanzania.

Wassalaam, Wenu Mwaminifu
Imesainiwa
Mirza Masroor Ahmad -
KHALIFATUL MASIH V

Ndoto 3 tukufu za Mtume Muhammad s.a.w

Kutoka uk. 1

kufa huwa hawarudi kimwili.
Hivi ndivyo yalivyo masimulizi ya safari za kindoto **za** Mtume Muhammad (saw), ile ya Mi'raji na ile ya Isra. Safari zile zilikuwa za kindoto siyo za kimwili. Baadhi ya waislamu wa baadae na hasa wanazuoni, kwa mapenzi ya upofu yaliyo pita kiasi na uvivu wa kutafakari mambo, bila ya kujitambua; waka zisimulia safari hizi kwa shangwe la ajabu sana. Wakazipamba ndoto hizi kwa taswira ya uhalisi wa kimwili na ufahu bayana. Maelezo yao juu ya safari hizi yanazisuta fahamu zao, kwa vile yamejaa viashiria vingi vya ndoto. Lakini kwa sababu ya kufunikwa na huba la upofuwa mapenzi juu ya Mtume (saw) ni ajabu kwamba, pamoja na viashiria vyote hivyo, bado wao wanashikilia na kung'ang'ania kwa nguvu zote kwamba, safari zile zilikuwa za kimwili halisi.

Kama ilivyo kwa Yule mkopesha deni ndotoni, ndugu wa marehemu huwawezi kulipa deni la namna ile, hata kama mdai ang'ang'anie kiasi gani! kwa sababu lile si deni halisi. Vivyo hivyo nasi, waislamu wa leo wenye tadaburi, hatuwezi kuendelea kusimulia safari zile kimazoea, na kung'ang'ania kuwa zilikuwa za kimwili halisi.

Kwa upevu wa fikra za kileo, utafiti wetu wa Aya kadhaa za Kurani Tukufu na vile viashiria vya ndoto, vilivyo jaa ndani ya masimulizi ya safari ya Mi'raji na Isra, vinatuthibitishia bayana kuwa, safari zile hazikuwa za kimwili bali za kindoto.

NDOTO HIZI ALIZIOTA LINI ?

Ndoto hizi tatu, Mtume (saw) hakuziota siku moja wala wakati mmoja, bali siku tofauti na nyakati tofauti.
Kwa mfano, ndoto ya kwanza - **safari ya Miraji. Hii** aliiota katika mwaka wa 5 (616) wa utume wake, akiwa mjini Makka nyumbani kwa Bi Khadija (ra). Ndoto hii imeelezwa Ndani ya Sura ya 53 (An-najim) aya ya 1-19.

Ndoto ya pili, ni ile **safari ya Isara. Ndoto** hii aliiota mwishoni mwa mwaka wa 10 au mwanzoni mwa mwaka wa 11 (620-621) wa utume wake, akiwa mjini Makka nyumbani kwa Umu Hani binti Abu Twalib, binamu yake. Ndoto hii, imetajwa ndani ya Kurani Tukufu sura ya 17, (Banii Israil) aya ya 2.
Ndoto ya tatu, ni safari ya **Kutufu Kaaba.** Ndoto hii aliiota akiwa mjini Madina, mwaka wa 6 Hijiria, yaani (628). Ndoto hii imelezwa ndani ya Kurani Tukufu, sura ya 48 (Al-Fata'h) aya ya 28-29. Ndoto zote hizi tatu zina umuhimu mkubwa kwa kila muislamu kuzifahamu na kuzielewa. Hadhi ya mtukufu Mtume Muhammad (saw),itabaki kuwa juu kwa kufahamu usahihi wa ndoto hizi.

1- NDOTO YA SAFARI YA MIRAJI – KUPAA MBINGUNI.

Hapa tuanze na ndoto yake ya kwanza – safari ya **Mi'raji.**
Mtume (saw), alisafiri kwenda Mi'raji, katika mwaka wa 5 wa utume wake. Katika safari hii ya kindoto, alijiona anapaa kwenda Mbinguni akiongozwa na Malaika Jibril a.s. Alisimulia ndoto hii kwa masahaba zake na kwa jamaa zake wa karibu. Katika masimulizi yake alisema kwamba, alimuona Malaika Jibril amemjia nyumani kwake usiku wa manane kwa kushuka kupitia paa la nyumba yake. Kisha Malaika huyu aliteremka na kumshika mkono, kisha akamtoa nje ya nyumba. Akaenda naye pembeni kidogo na kumlaza chini shemu fulani. Hapo chini akaanza kumchana kifua chake na kuutoa moyo; kisha kausafisha kwa maji ya Zam zam. Baada ya hapo Malaika Jibril akakileta chano cha dhahabu na bakuli **ililo jaa Hekima na imani, na kuimimina hekima ile katika kifua chake na kukifunga**. *Je hekima na imani ni vitu vya kuteka na kumimina kama yalivyo maji au maziwa?* ***Tafakari.***

Baada ya tukio hili la upasuaji, mtume s.a.w anasimulia kuwa, safari ya **kupaa kwenda mbinguni** ikaanza, ikiongozwa na Malaika Jibrili. Walipofika mbinguni, Malaika Jibril alimuongoza na kumuingiza kila mbingu, tangu ya kwanza hadi ya saba. Kila mbingu waliyo ingia walikuta Lango na walinzi. *Je mbingu imejengwa kama zilivyo nyumba za ghorofa za kidunia? Tafakari*.

Katika kila mbingu Malaika Jibril alikuwa, **akimtambulisha Mtume s.a.w kwa nabii aliye mwenyeji wa mbingu hiyo.** Walizimaliza mbigu zile saba, kisha Mtume s.a.w, akapelekwa katika kituo kiitwacho ***Sidrata Muntaha***. Kule katika Sidrati Muntaha Mtume s.a.w, alifanya **mazungumzo ya ana kwa ana na Allah. Kisha akapewa amri na Allah ya kusimamisha sala Hamsini kwa siku, yeye na umati wake**.

Mtume s.a.w, anaendelea kusimulia kwamba, alipokuwa akirudi kutoka Sidrat Muntaha, njiani katika **mbingu ya sita alikutana na nabii Musa a.s,** akamuuliza ni amri gani aliyopewa na Allah? Mtume s.a.w. akajibu nimepewa amri ya kusali sala Hamsini kwa siku. *Je walielewanaje kilugha na hali wao ni makabilamawili tofauti? Tafakari.* Nabii Musa akaniambia kuwa watu wako hawataweza kutimiza amri hiyo. Rudi kwa Mola wako ukamuombe akupunguzie



Ustadhi A .R. Mikila

idadi ya sala. Mtume s.a.w. anasema alirudi kwa Allah, akaomba kumpunguziwa idadi ya sala na Allah Akakubali Akampunguzia. Nilipofika tena kwa nabii Musa aliniuliza, sasa umepewa kiasi gani cha sala, nilipo kitaja kile kiasi, nabii Musa bado alikiona ni kikubwa, akanishauri tena kurudi kwa Allah, kuomba kupunguziwa tena. Hali hii ya nenda rudi iliendelea na hata kuzidi. Hatimaye punguzo likafikia sala tano. Hata idadi hiyo Nabii Musa bado aliiona ni kubwa. Kwa mara nyingine alinishauri nirudi tena kwaAllah, nikaombe kupunguziwa zaidi. Mtume (saw), anasema katika masimulizi yake kuwa,

hapo nikamwambia nabii Musa kwamba, sasa naona haya kurudi tena kwa Allah kuomba hili. Kisha Mtume s.a.w, anasema akaingizwa Peponi na humo akaziona kuta za Pepo zime pambwa kwa Vito vya Lulu na ardhi yake inamanukato ya Miski. *Je, Pepo ni kituo cha utalii, mtu huingia na kutoka? Tafakari.*
Maelezo ya safari hii ya Mi'raji, yanapatikana katika kitabu maarufu cha Imam Bukhari, katika malango wa sala na mlango wa utukufu wa mitume. Msimuliaji wa hadithi ni Anas bin Maliki r.a, sahaba maarufu sana wa Mtume (saw).

SAFARI YA MI'RAJI KUWA YA KINDOTO.

Zipo sababu nyingi zinazo ifanya safari ile iwe ya kindoto zaidi kuliko kuwa ya kimwili. Hapa nitazieleza sababu chache za hali hiyo.

SIFA ZA NDOTO

Ndoto inazo sifa maalum zinazo itambulisha kuwepo kwake.
Kwanza - ndoto hutokea usingizini mtu alalapo, iwe usiku au mchana**.**
Tukio hili la safari ya Miraji, lilitokea usiku wa manane Mtume s.a.w, akiwa amelala.
Pili - muota ndoto huwa ni mmoja peke yake, na ndiye msimuliaji wa alicho ona na kushiriki humo ndotoni.
Msimuliaji wa safari hii ya Miraji ni Mtume s.a.w, peke yake. Watu wa nyumbani mwake hawakujua lolote wala hawakuona chochote cha kustajabisha.
Tatu - katika ndoto matukio huungwa ungwa, haliwi jambo moja tu la kuonyeshwa.

- Katika usiku ule wa Miraji, Malaika Jibril alionekana kuingia nyumbani kwa Mtume (saw), kupitia juu ya paa la nyumba, kinyume na kawaida yake. Wala hakutoa salamu kwa Mtume (saw), wala hakuzungumza naye lolote. Shughuli ya upasuaji wa kifua chake hadi kutolewa moyo, haikumsitua Mtume s.a.w, wala upasuaji ule haukumpoteza fahamu. Matendo yote hayo aliyaona, tena hatua kwa hatua kana kwamba aliyekuwa anafanyiwa upasuaji ule ni mtu mwingine.

Nne - Muda wa kuona ndoto huwa ni mfupi, yaani huchukuwa dakika au saa chache tu kumalizika.
- Mamboyaleyaupasuaji, kupaa mbinguni, kuingia kila mbingu, kusalimiana na Mitume alio wakuta mbinguni, kwenda kwake Sidrat Muntaha, kufanya maongezi ya ana kwa ana naAllah; kubadilishana taarifa na nabii Musa (as), ya idadi za sala na kurudi tena Makka kabla ya alfajri, yote hayo yalifanyika usiku kwa

usiku kwa saa chache tu.

Tano - muota ndoto hujiona katika uhalisia wa kumshangaza sana.
- Tendo la kufanyiwa upasuaji na kutolewa moyo huku akiwa anaona, *hili ni jambo la kushangaza*. Kule kupaa angani bila ya mbawa, kuona Mbingu ikiwa ni makazi ya watu na manabii wachache, *nalo ni jambo la kushangaza*. Kuongea kwake na manabii, hasa nabii Musa na kuelewana naye kilugha bila mkalimani, yote hayo *ni mabo ya kushangaza* na ni kinyume cha mazowea.
Sita - Ndoto hutenda jambo lisilo wezekana kutendeka katika hali ya kawaida,

- Mtume (saw), alipaishwa kwenda mbinguni bila mbawa, alipasuliwa kifua chake bila kisu, akatolewa moyo bila kupata jaraha. Kifua chake kiliunganishwa bila nyuzi. Aliingia peponi na kutoka kama mtalii. Mtume s.a.w, alipokea ushari wa kupinga kutekeleza amri halali aliyopewa na Mola wake ya kusali sala Hamsini kwa siku; kadhalika kuongea na mitume walio kufa zamani. Yote hayo yaliwezekana kwa sababu ilikuwa ni ndoto.
Saba - Ndoto huanzia usingizini na huishia usingizini**.**

- Mtume s.a.w, alipo amka usingizini, hakuliona lile jaraha la upasuaji au alama yoyote ya mshono kifuani kwake. Hakuona uwazi juu ya paa la nyumba yake. Alijiona yupo nyumbani mwake, kitandani kwake, wala hana uchofu wowote wa safari. Yote hayo yalikuwa ya ndotoni na yaliishia ndotoni humo humo.
Nane - Ndoto haina shahidi wa tukio linalo simuliwa.

- Mtume s.a.w, alipo simulia safari yake ya Miraji, hakuna mtu aliye hitaji ushahidi wa tukio hilo, ama kutoka kwake au kwa watu walio kuwamo nyumbani mwake usiku ule. Watu hawakuhitaji kuthibitisha ukweli wa safari ile ya ajabu. Wale walio simuliwa habari ile walielewa kuwa wanasimuliwa mambo ya ndoto. Hawakuhitaji hata maana ya ndoto yenyewe.

Tukiyachunguza kwa makini masimulizi yote ya safari hii ya Mi'raji, tutayaona ni kwa kiasi gani yanagusa sifa za ndoto nilizo ziorodhesha hapo juu. Masimulizi yaliyomo ndani ya vitabu vya hadithi za Mtume (saw), yanayo husu safari hii ya Mi'raji; yanathibitisha wazi wazi kuwa safari nzima ilikuwa katika hali ya ndoto, mbali kabisa na dhana ya kwamba safari ile ilikuwa ni ya kimwili halisi na ufahamu bayana.
Hebu tuyaangalie madokezo ya kindoto, yanayo onekana katika safari hii ya Mi'raji.

1- Safari ile ilianza usiku wa manane, na kiongozi wa safari alikuwa Malaika Jibril mwenye mbawa za kurukia.
- Mtumeme s.a.w hakuwa na mbawa, hivyo asingeweza kuruka. Lakini kwa sabu ya ndoto alijiona anaruka.

2- Safari hii ilikuwa ni ya usiku wa manane, mtume alikuwa amelala.
- Lakini ndotoni alijiona yuu macho hata kuweza kuyaona yote aliyo fanyiwa na Jibril. Kama vile upasuaji wa kifua chake, moyo wake kutolewa na ule usafishaji wake na hata kurudishwa tena mwilini. Kindoto yote hayo yaliwezekana.

3- kwenda mbinguni kimwili na kurudi duniani.
- Jambo hili halimo katika maisha ya kawaida yaliyo zoeleka ya mwana damu. Eneo hili la mbingu ni daraja tu la kiroho, katu haliwezi huwa na majengo ya kidunia. lakini kindoto yeye aliyaona majengo ya peponi na hata aliweza kuingia humo na kutoka.

4- Kuwaona Mitume walio kufa zamani wakiwa hai, wanaongea na kubadilishana naye mawazo na kupeana ushauri bila mkalimani. -
Jambo hili nalo linawezekana ndotoni tu, lakini katika uhalisia haliwezekani.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Kazi ya kuitangaza Islam ni ya Ahmadiyya pekee - Asema Khalifa Mtukufu a.t.b.a.

Na Dawati la Kiswahili
Morogoro

Hotuba ya leo pia, ni mlolongo wa hotuba zilizotangulia. Leo yataelezwa yale mambo mawili muhimu, yenye kutoa haki za jamii, yenye kumaliza fitna na ufisadi katika jamii, yenye kueneza amani na usalama ndani ya jamii, yenye kustawisha haki na uadilifu ndani ya jamii, na kuyafuata kwa moyo, maagizo ya Mwenyezi Mungu. Na yenye kutoa mwanga kuhusiana na kuzitimiza ahadi zenu au kuhusiana humo na Qur'an Tukufu imevyoelezwa kama nilivyoeleza.

Leo islam inalalamikiwa kwamba, Mungu Apishe mbali, mafundisho yake ni makali, kwamba hakuna chochote humo mbali ya ugaidi na kueneza fitna na ufisadi.Siku chache tu zilizopita, mwandishi fulani wa Kimarekani aliandika kwamba, siku ya Ijumaa, ndani ya Islamu, ni siku ya ufisadi, na ameandika mambo kadhaa dhidi ya Islam.

Jumuiya imewasiliana naye, na kijana wetu fulani akaandika madhumuni nzuri sana kuhusiana na uzuri wa Islam. Baada ya kuwasiliana naye zaidi, nikaagiza kwamba madhumuni zaidi ya aina hii, yahusikanayo na uzuri wa Islam na yale mafundisho mazuri ya Islam, yale makusudio ya Islam, yale makusudio ya Ijumaa, yaandikwe zaidi ili watu wapate kufahamu.

Leo, kazi hii ni ya Jumuiya ya (Waislamu wa) Ahmadiyya tu, Jumuiya yenye mapenzi ya kweli ya Mtume s.a.w. ikiiendeleza kazi yake, sio tu kwa kuihami Islam na mashambulizi inayofanyiwa, bali kwakuufunga pia mdomo wa adui kwa hoja na dalili.Kwa hali yoyote ile, hili ni jukumu letu, lakini Mwenyezi Mungu Mwenyewe Ameuandaa mpango.

Wakati mwingine huwasimamisha hata wale wasiokuwa Waislamu, wenye kupenda uadilifu, ambao huelezea uzuri wa Islam. Matokeo yake ni kwamba, kuna mkristo fulani wa kikatoliki aliye mwanazuoni, akiwa ni Profesa wa Chuo Kikuu, ambaye aliandika, katika siku zilizopita, madhumuni fulani, ndani ya gazeti la Daily Telegraph, ambamo ameisifu Islamu na Waislamu, na kuvipinga vile vikundi vya hapa vyenye kuendekeza ubaguzi wa kikaumu, na akaandika hivi kwamba zile historia na mafundisho ya hali ya juu ya waislamu, yanapaswa kustawishwa.

Siku hizi wengi wa wale wenye kuzilaumu dini na Islam ni hawa hawa watu wenye kuukana uwepo wa Mwenyezi Mungu. Kwa vyovyote vile, kama nilivyosema, kwamba kazi hii leo ni yetu. Tuithibitishe haja ya kuwepo kwa dini na kuithibitishia dunia uwepo wa Mungu Aliye Hai, kwa sababu ni mwislamu tu wa kweli awezaye kuitekeleza kazi hii. Na baada ya kuachana na Imamu wa zama, basi ni Waahmadiyya tu ndio wenye kuyaelewa mafundisho sahihi ya Islam na kuyaeneza duniani humu. Na inapaswa iwe hivyo, na kazi hii inawezekana tu kwa kuyatekeleza mafundisho na maagizo ya Qur'an Tukufu.

Kama nilivyosema kwamba, leo nitaongelea kilekinachohusiana na amri zile mbili zimezotajwa katika orodha ile ya sura ya An aam aya za 152 – 153, ambazo nimekuwa nikizitaja katika hotuba chache zilizopita.

Miongoni mwa mambo yatakayoelezwa leo, jambo la kwanza linahusiana na haki na uadilifu. Allah Anasema: *Wa idhaa qultum fa'diluu wa law kaana dhaa qurba* Na msemapo basi mseme jambo la uadilifu hata kama mtu huyo unaye sema naye ni jamaa yako wa karibu kiasi gani.

Uadilifu una sura tofauti, na kuhusiana na jambo hili, kuna maagizo pia ya ufafanuzi katika sehemu tofauti ndani ya Qur'an Tukufu. Ushahidi ule utolewao kwa jamaa wa karibu, Mwenyezi Mungu Ameufafanua zaidi sehemu nyingine kwa kusema kuwa, sio tu kwa jamaa wa karibu, bali Amemjumuisha hata mwenyewe mwenye kutoa ushahidi na kuwajumuisha pia hata wazazi.

Ni katika aya ya 136 ya Sura ya An Nisaa ambamo Allah Ta'ala Anasema: *Yaa ayyuhal ladhiina aamanuu kuunuu qawwaamiina bil qistwi shuhadaa a lillaahi walaw 'alaa anfusikum awil waalidaini wal aqrabiin, in yakun ghaniyyan au faqiiran fallaahu Awlaa bihimaa, falaa tattabi'ul hawaa an ta'adiluu, wa in talwuu aw tu'uridhwuu fainnal Laaha kaana bimaa ta'amaluuna Khabiira* yaani:

Enyi watu mlioamini, mkiwa mashahidi kwa ajili ya Allah, kuweni wenye kuustawisha uadilifu kwa nguvu sana, hata kama mlazimike kutoa ushahidi dhidi yenu wenyewe au dhidi ya wazazi au dhidi ya ndugu wa karibu, awe tajiri au masikini, Allah ni mwangalizi bora wa wote hao. Hivyo msiyafuate matamanio yenu, msiuepuke uadilifu. Na kama mtatoa kauli iliyopinda kwa kuuepuka upande huu, basi kwa yakini Allah ni mwenye kuyajua sana myafanyayo.

Hapa jambo la msingi limeelezwa kuhusiana na ushahidi, kwamba shuhuda zenu zitolewe tu kwa ajili ya kupata radhi ya Mwenyezi Mungu, na ziwe zenye kufuata amri za Mwenyezi Mungu. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema sehemu fulani kwamba:'simameni kwenye haki na uadilifu na inapaswa kila ushahidi wenu uwe kwa ajili tu ya Mwenyezi Mungu. Hivyo duniani kuna njia moja tu ya kustawisha uadilifu na haki, kwamba kusudio liwe la kupata radhi ya Allah. Mbali na hiyo kiwango kile cha juu hakiwezi asilan kuwepo chenye kuweza kumaliza makusudio ya kidunia na ya kibinafsi.

Kama maelezo ya aya hii yameyotolewa yatekelezwe, yaani kwa ajili ya kustawisha uadilifu, mwanadamu asisite hata kutoa ushahidi dhidi yake binafsi, asisite hata kutoa ushahidi dhidi ya wazazi wake na hata asiache kutoa ushahidi dhidi ya ndugu wa karibu, basi hapo jamii nzuri hustawi ambao mfano wake hauwezi kupatikana.

Haja ya ushahidi hupatikana wakati masuala kati ya pande mbili yapatikanapo. Kwa sura ya aina hii, au pande hizo mbili zinapoambiwa zijieleze, aidha watolewapo baadhi ya mashahidi, ili uhakika wa mambo uwe wazi, na wepesi upatikane katika kutoa uamuzi na kustawisha uadilifu na haki. Kama shuhuda ziwe za uwongo, kwa kutoa maelezo yaliyopinda kwa ajili ya kuipata haki isiyojuzu, basi hata uamuzi wa mtoa uamuzi pia unaweza ukawa sio sahihi, na sio tu usio sahihi bali wakati mwingine unaweza kuwa wenye makosa makubwa sana, na hivyo, katika sura hii, dhambi inakuwa juu ya vichwa vya watoao ushahidi, haiwi juu ya watoao uamuzi.

Baadhi ya shuhuda haziwi kwa ajili ya kujinufaisha, bali hutolewa kwa ajili ya kuwanufaisha wapendwa wake, hujaribu kuiongoza idara inayotoa maamuzi kwenye njia potofu na halafu matokeo yake wanakuwa ni wenye madhambi.

Naam, Mtume s.a.w. alisema: kama yeyote atoe maelezo potofu na kunifanya nitoe uamuzi usio sahihi, basi huwa inakuwa kama mimi ninampatia kipande cha moto. Hivyo kila mmoja anapaswa ajiepushe kupata kipande cha moto kwa kutotoa maelezo ya uwongo na ushahidi wa uwongo. Mwaminio wa kweli ni yule anayejiepusha nayo.

Aya ya Sura ya Annisaa niliyoisoma ina maagizo ya mambo makubwa, hivyo kama watu hao, wanaojitahidi kuzichukua haki zao kwa njia isiyojuzu, awe mume au mke, kwa namna hii hii, katika sura ya Talaka au ya khula, ndugu na marafiki wa mume au mke, wakitoa ushahidi usio sahihi wakijaribu kupata baadhi ya faida zisizojuzu, hao wanauua uadilifu.

Kwa namna hii hupata faida za muda mfupi tu za kidunia, lakini hicho wakichukuacho ni kipande cha moto, kama vile Mtume s.a.w. alivyosema, ambacho siku ya kiama kitawepeleka kwenye matokeo mabaya. Allah Taala Anasema kwamba pande zote mbili na hata pia wale watoao ushahidi, kwa kuyafuata matamanio yao, taratibu wanaenda mbali na uadilifu. Hivyo badala ya kuyafuata matamanio, tendeni haki na uadilifu.

Kisha Allah Anasema: "*wa in talwuu au tuuridhuu, fainallaaha kaanabimaataamaluunakhabiraa*"; yaani kama mkisema kauli isiyonyooka, au mkikengeuka, basi Allah Anazo habari za yale mnayoyatenda. Hivyo basi, ushuhuda wa uwongo unaweza kumdanganya hakimu au yule aliyepewa jukumu la kukata shauri na kuyageuza matokeo, lakini hauwezi katu kumdanganya Allah Aliye na habari zote.

Mtume Muhammad saw alielekeza, kwa msisitizo mkubwa, kwenye kusema kauli safi iliyonyooka, kwa kuliweka agizo hili la Mwenyezi Mungu katika hutuba ya ndoa. Mtume saw alihimiza sana kwamba wakati wa kufunga ndoa, (wanandoa wanatakiwa) waishi hivi kwamba wakati linapotokea tatizo lolote, daima mfuate agizo la "quuluu qaulan sadidan" (semeni kauli iliyonyooka). Kuachana na kusema kauli iliyonyooka kutawapelekeni mbali na taqwa au kutawapelekeni mbali na haki na uadilifu na kuwa chanzo cha kusababisha fitina na ufisadi katika jamii.

Katika idara yetu ya Jumuiyya iitwayo "qadhaa", kesi za khula na talaka zinapoletwa, ambazo baadhi yao naziangalia mwenyewe, kwamba watu hawasemi kauli iliyofungamana na uhakika na uadilifu, wala mashahidi hawatoi shuhuda za kweli. Halikadhalika kuna masuala ya kupokea na kutoa, na hata katika masuala hayo, wengine wanakula moto kwa kujipatia masilahi binafsi na ya muda, kwa kwenda mbali na taqwa.

Hadithi ielezayo habari za kula moto inataja milki ya ndugu wawili waliokuja mbele ya Mtume Muhammad saw, naye akasema hodari zaidi wa kutumia maneno anaweza kunifanya nikate shauri apendavyo, lakini atakuwa anapata moto kutoka kwangu na kitendo chake hiki kitageuka kuwa mnyororo shingoni mwake siku ya kiama. Baada ya kuyasikia maneno haya , ndugu wote wawili wakaanza kulia na kusema kuwa hatutaki cho chote. Kila mmoja alitaka kuacha haki yake na kumpatia ndugu yake.

Hapo Mtume saw akasema kwamba kuacha haki pia ni kosa na kila mmoja wenu ana haki na aichukue haki yake, na kama mnashindwa kuamua kutokana na ukosefu wa ushahidi wa nyaraka auwa mashahidi, basi mkapige kura na cho chote mnachobahatika kukipata mkakichukue.

Basi hii ndiyo njia ya kuhukumu kesi na hiki ndicho kiwango cha taqwa ambacho mwislamu anapaswa kuwa nacho. Mwenyezi Mungu Awarehemu na kuwapa akili watu wa namna hii ambao wanakuwa kikwazo katika kufanya uadilifu. Kama katika masuala ya nyumbani na ya biashara, zitolewe shuhuda za kweli ili kufanya uadilifu, basi jamii yetu inaweza kutoa mfano wa pepo(jannat) hapa duniani.

Kama nilivyotangulia kusema kwamba katika Qurani Tukufu mna maagizo ya kina yahusikanayo na uadilifu. Kuhusiana na hilo ningependa kuweka mbele yenu aya mbili tatu zaidi.

Allah Taala Anasema katika sura Annisa "*innallaaha yaamurukum an tuaddul amaanaati ila ahlihaa wa idhaa hakamtum bainannaasi an tahkumuu bil 'adli, innallaaha ni 'imaa ya'idhukum bihi, innallaaha kaana samiian baswiraa*"yaani,kwayakiniAllah Anawaamuruni kuwakabidhi amana wanaozistahili na mnapohukumu baina ya watu basi hukumuni kwa uadilifu. Bila shaka ni mazuri sana Anayowasihini Allah. Hakika Allah ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.

Jambo la kwanza lililotajwa katika aya hii ni kuwakabidhi amana wanaozistahili, na juu ya hilo nilisha toa tayari hotuba ndefu, kwamba mwaka huu ni mwaka wa kuwachagua viongozi (wa Jumuiyya). Kwa hiyo, kwa kuyaweka kando matamnio binafsi, ujamaa na undugu, chagueni kwa uadilifu na kutimiza haki ya amana (kwa kuweza kupata) viongozi wanaoweza kutekeleza wajibu wao vizuri. Kwa vyovyote vile, chaguzi zimekwisha fanyika na katika baadhi ya jamaati, watu wenyewe waliwachagua viongozi wachapakazi na katika baadhi ya jamati nilifanya mabadiliko au sikukubaliana na mashauri ya wenye kutoa mashauri,bali yule aliyekuwa akifanya kazi

Endelea uk. 7

Bustani ya Washairi

Neno la kwanza la Allah kwa mbora wa viumbe, Bwana mwenye daraja, sirajal munira, khataman Nabiyyin lilikuwa SOMA. Ni vigumu kumtambua Allah bila kusoma. Huo ni wajibu kwetu. Sheikh Kaluta Amri Abedi anatuhimiza.

1 Jinale nalikadimu, Mola aturehemuo
Sifa yake ni alimu, kwake hakuna upeo
Yeye chanzo cha elimu, mambo hufanya kwa hio
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

2 Mjinga na Mualimu, hawawi walinganao
Mfano chungu na tamu, kwao wafananishao
Mzima na mjuzamu, uwapo usawa wao?
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

3 Mjuzi anafahamu, mambo kwa vituo vyao
Watu wanamuheshimu, heshima impasao
Uongozi wa kaumu, ni haki ya wajuao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

4 Wajinga watungurumu, kamwe si watambuao
Mepesi kwao magumu, sio wapambanuao
Wapigie baragumu, wao si wasikiao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

5 Ujuzi jambo adhimu, unayo mengi mafao
Pambo la kweli elimu, kwa mtu limpambao
Hukuinua makamu, ukawa mtukuzwao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

6 Mjinga na uhasimu, ndio hudarana nao
Mithili ya pakashumu, kwa jeuri na uamio
Au kama dhilighamu, afanyapo shambulio
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

7 Taji la mwenye elimu, ni taji mahitajio
Huzitawala kaumu, bila mikuki na ngao
Amrize zikatimu, kwa wema na maridhio
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

8 Ukisikia elimu, mradi ni dhamirio
Nahitaji kukuhimu, kwa dunia ni dinio
Shule zifanyie hamu, kuelimisha wanao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

9 Khasa kwa waislamu, ni jambo la mshangao
Vile hawana elimu, imeshuka hadhi yao
Hafifu duni adimu, yanywea majina yao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

10 Na mijini ndimo humu, yalimo yao makao
Vyeo hasa mahashumu, walahi haviko kwao
Vyashikwa wenye elimu, vijijini watokao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

11 Ofisi zote za humu, vyeo vikuu si vyao
Ujumbe ni yao hamu, na utarishi ni wao
Na uboi ya salamu, ndio hujisifu nao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

12 Na dini hawafahamu, hiyo wajisifiyao
Hata kutayamamu, ni wachache wajuao
Vile hawana elimu, Mola sio wamchao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

13 Wapendavyo maadhimu, na michezo kama bao
Zimewatoka fahamu, hawahisi dhila yao
Na wete kwenye elimu, wakisia mengineo
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

14 Haya shime na elimu, chonde mnisikiyao
Tuikoe kaumu, ya watu waaminio
Ukue Uislamu, watukuke tuzaao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

15 Beti zangu zimetimu, kitim cha wajuao
Kazaneni na elimu, mpate maendeleo
Sasa natua kalamu, ya ushinde ushindao
Watumishi wamchao, Mola ni wenye elimu

Nae Al-Ustadh Hamisi Sultani Wamwera anaogelea katika bahari hiyo hiyo ya Mwalimu wake na anaelekeza fikra zetu kwa shule yetu ya Kitonga. Na anasema hiyo itatimiza haja yetu ya kupata elimu.

1 Bismillahi Sayyidi, Mmoja hanaye mama
Hana baba yu Wahidi, yu hivyo dumu daima
Vyote vinamsujudi, kwa khushui hutetema
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

2 Andiko langu sadidi, mudili kwako natuma
Lishufu kama shadidi, litoe sila husuma
Ni ombi kwake Wadudi, shule aipe iqama
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

3 Allah ninakuhimidi, pekee kwa taadhima
Weye ndiye maujudi, mjuzi mwenye huruma
Mjumbeo Muhammadi, ulimfunza kusoma
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

4 Tumechelewa zaidi, wenzetu wali mapema
sasa nasi kwa udodi, nia yetu kwenda hima
Utuongeze sipidi, kusomesha na kusoma
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

5 Sigani kitajuwidi, ni ombi kwako Rahima
Nakuomba makusudi, shule isitawi thumma
Ijulike kwa idadi, wataofaulu vyema
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

6 Elimu ni zumaridi, kuitafuta lazima
Hata ikiwa baidi, twende pawapo salama
Wajibu na inabidi, kwa waume na wamama
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

7 Elimu nairadidi, marashi ya riha njema
Ni uturi ndio udi, mtu huwa akhalama
Kuipata ninakidi, hata kwa gani gharama
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

8 Nikiwa kama junudi, wa jeshi la Islama
Shule yetu nainadi, ipo juu ya mlima
Ya mazingira ukudi, mazuri yaliyo mema
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

9 Shule hino maridadi, walimu wanajituma
Ni walimu weledi, watapaka zao wema
Kwa bidii na juhudi, wepesi si wa kukwama
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

10 Wana ari ya fuadi, na m oyo wa kujituma
Wote wafanya jihadi, kufundisha bila ngama
Mola wazidishe mudi, wasije wakatuhama
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

11 Waliyoko kwenye bodi, Rabbi uwape hekima
Sana wanajitahidi, shule iwe ya heshima
Wajazi ilimuradi, wasiwe mwamazumuma
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

12 Kwa waalimu na bodi, kwa mimi ninavyopima
Shule itapanda hadi, kuwa sawa na mlima
Ewe Mola tuahidi, ndoto yetu iwe kama
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

13 Ili shule kuwe idi, sherehe kuunguruma
Vijana mjitahidi, masomo yenu kusoma
Ombeni kwa kusujudi, Mwenyezi Mungu karima
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

14 Msiwe mithili radi, pulikizeni daima
Msifanye ukaidi, mwalimu akiwasema
Ridhini akiwarudi, nidhamu kitu adhima
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

15 Ujeuri si samadi, si mbolea ilo njema
Ninyi ni wataradadi, walimu wape heshima
Japo kimo na jasadi, msawa mkisimama
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

16 Wazazi wa auladi, msibaki nyumanyuma
Leteni wana wafidi, wafaidike kusoma
Ewe mlezi faidi, tumia hii neema
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

17 Karo si kubwa zaidi, yaendana na ya umma
Ukitaka ushahidi, enenda shuleni hima
Utapatwa na butadi, ipo nafuu kwa umma
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

18 Kumi na nane sizidi, hapa natamka tama
Kusudio na muradi, nahisi nimetuama
Penye kosa na inadi, ni mie mwenye lawama
Shule yetu ya Kitonga, iwe moja ya mfano

K - mtoto (Abdallah Said Kalindima kasema mambo mazito, mithili mafuta ya uto. Beti zake ni dawa za kutufanya tutafakari. Ada ya mja hunena muungwana ni vitendo.

(Limeambatanishwa)

Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe, bilkhususi ukuta huo ukiwa umejengwa kwa amri ya Muumba wa mbingu na ardhi, Anayesimamisha mbingu hii bila nguzo tunazoziona. Wengi wameumia waliojaribu. Mmoja aliyojitoma kwa uzembe ni Sheikh Yahya Hussein. Akiwa Nairobi alianzisha gazeti alililiita TAA. Masikini Taa ya Sheikh wetu huyo haikuwa Taa ya maana bali kibatari na mara ilizima kwa upepo wa Askari wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Upepo ulivumishwa na Sheikh Amri aliyesema;

1 Taa la Sheikh Yahya, ni taa la kibatari
Lenye moshi ya kayaya, ya uzushi na batari
Lenye utovu wa haya, na kina cha ujahiri
Taa lao kibatari, huzima na mpepea

2 Naapa Mola Jalia, Alomtuma Rasuli
Ninyi mtatukimbia, katika hiki kitali
Hodari kushambulia, silaha yetu ukweli
Taa lao kibatari, huzima na mpepea

3 Tuna panga asilia, zenye makali kuwili
Ni aya zake Jalia, na hadithi za Rasuli
Watu wema hutulia, tuhojipo kwa dalili
Taa lao kibatari, huzima na mpepea

4 Tahofuje khunsia, hali sisi ni rijali
Na lije kwa kutishia, kundi la hao juhali
Watajuta na kulia, kwa pigo lilivyo kali
Taa lao kibatari, huzima na mpepea

5 Wangapi walikithia, wanatuzidi hali
Walipotukurubia, tukawafanya dhalili
Sasa wameshafifia, zimewanywea kauli
Taa lao kibatari, huzima na mpepea

6 Shindo limewaishia, zimewapotea hali
Hawa wanaowaunia, wale wanawakejeli
Kokote yawavizia, ikabu yake Jalali
Taa lao kibatari, huzima na mpepea

7 Haki ni Ahmadia, uislamu wa kweli
Wote wanadidimia, wapinzao kwa fedhuli
Wote wanainukia, wema wenye kukubali
Taa lao kibatari, huzima na mpepea

Nae Mzungu mmoja maarufu na bingwa wa Kiswahili Sheikh Lambert alikebehi Taa ya Sheikh Yahya na kucheka. Anasema;

Mwangaza ulo mzuri, ndio wenye kung'ariza
Dhalamu zilo dhamiri, ziwezazo kupoteza
Uonyeshayo dhahiri, zitazo tuendeleza
Taa isoshinda giza, haina maana kamwe.

Kazi ya kuitangaza Islam ni ya Ahmadiyya pekee

Kutoka uk. 5

vizuri akaruhusiwa kuendelea.
Utendaji wa kazi una kiwango chake maalum, na vipawa vya mtu vinapokifikia kile kiwango, hapo idara hiyohukosa tena maendeleo. Na yawezekana kwamba mtu fulani aliyeshindwa kufanya kazi vizuri katika idara fulani angefanya vizuri katika sehemu nyingine. Kwa sababu hiyo pia, mabadiliko kadhaaa yalifanywa. Wengine wanafikiri kwamba mabadiliko ya baadhi ya watu yamefanyika kutokana na kuwachukia, ilhali manufaa ya Jumuiyya yamepewa kipaumbele zaidi kuliko chuki.
Popote pale nilipohisi kufanya mabadiliko niliyafanya kwa kutimiza haki ya uadilifu. Allah ndiye Ajuaye yaliyomo vifuani, na sisi tunaweza kuhukumu na kushauri kitu kwa kuangalia tu hali ya dhahiri.Lakini, hata hivyo, katika jamaati kadhaa za baadhi ya nchi, viongozi wamechaguliwa kwa kuzingatia ujamaa, undugu na uhusiano wa karibu. Mwenyezi Mungu Awarehemu na kuwapa akili watu hawa, ambao wanayatanguliza matamanio yao binafsi juu ya uadilifu.
Sasa wajibu wa wale waliochaguliwa kuwa viongozi ni kwamba, wakimweleza Allah udhaifu wao, wamwombe ghofira na msaada na wayatekeleze majukumu yao kwa uadilifu. Uongozi unapaswa kuthaminiwa, maana uongozi ni neema na fadhili ya Mwenyezi Mungu. Sasa jitahidini kufanya uadilifu katika kuwaleawanajumuiyya, kuwatendea wema, kutatua matatizo yao na kupanga mipango yenye kuleta maendeleo ya Jumuiyya. Sasa jitahidini kuitimiza haki ya kufanya kazi kwa bidii, kwani masharti yote ya agizo hili la" *tahkumuu bil 'adli*" (hukumuni kwa uadilifu), yatatimizwa pindi mtakapotekeleza wajibu wenu wa kuitumuikia dini kwa vipawa na nguvu zenu zote. Na kila kiongozi, awe wa jamaati ndogo au awe kiongozi wa kitaifa, anapaswa kuyazingatia mambo haya. Manufaa ya Jumuiyya yatangulizwe juu ya manufaa yoyote ya binafsi,waila Mwenyezi Mungu Anavitazama vitendo vyetu kila sekunde na kuvihesabu.
Hivyo basi, kila kiongozi aliyechaguliwa au aliyeteuliwa, ajitahidi kuitekeleza kazi hii ya kuitumikia dini, akiamini kuwa ni fadhili ya Mwenyezi Mungu. Bila shaka Allah Atawahoji viongozi wa kidunia pia, lakini kama wale wanaochaguliwa, kwa jina la Allah, kufanya kazi yoyote, hawatimizi haki ya amana zao, na kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu na haki, basi watahojiwa zaidi kuliko viongozi wa kidunia. Basi kila mmoja ajitahidi kutekeleza majukumu yake akifanya istighfar na kuomba msaada na kuonesha unyenyekevu. Allah Awawezeshe viongozi wote na watumishi wote wa Jumuiyya kutekeleza majukumu yao barabara.

Kisha twaona kwamba, baada ya kupata mwongozo katika maisha ya kinyumbani na masuala ya kibiashara na utekelezaji wa majukumu ya viongozi, Islam inatoa amri gani zaidi kwa ajili ya kustawisha uadilifu. Kuna amri moja ambayo ni dhamana ya kustawisha uadilifu na amani duniani. Allah Anabainisha katika aya ya tisa ya Sura Almaeda

Yaa ayyuhal ladhiina aamanuu, kuunuu qawwaamiina lillaahi, shuhadaa a bil qistwi, walaa yajrimannakum shana aanu qawmin 'alaa allaa ta'adiluu, i'idiluu huwa aqrabu lit taqwaa, wattaqul laaha, innal laaha khabiirum bimaa ta'amaluun.
Yaani:'enyi mlioamini! kuweni wasimamizi kwa ajili ya Allah, mtoao ushahidi kwa uadilifu, na uadui wa kaumu yoyote usiwashawishini kwamba msifanye uadilifu, fanyeni uadilifu, huo ni karibu sana na taqwa, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu daima Anazo habari za yale mnayoyatenda.'
Tazameni kwamba mafundisho haya ni mazuri kiasi gani kwa kuondolea mbali fitina na ufisadi duniani. Wanaoisingizia dini tukufu ya kiislamu hawawezi kutoa mfano wa mafundisho haya mazuri kutoka katika mafundisho yao ya kidunia na ya kidini. Mwenezi Mungu Anawaambia waaminio kwamba " *kuunuu qawwaamiina lillaahi*":kuweni wasimamizi kwa ajili ya Allah.
Qawwaam maana yake ni mtu anayeendelea kufanya kazi yake kwa njia iliyo bora bila kuacha kasoro yoyote. Hivyo basi, mwaminio wa kweli anayefanya kazi, hufanya kazi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kujitahidi kujiepusha na uzembe, ulegevu na kutawaliwa na matamnio yake binafsi.
Kazi ya mwaminio ni kwamba atoe shahada kwa kuunga mkono na kwa uadilifu, na kiwango chenyewe cha uadilifu ni kipi?Kiwango cha uadilifu si kutenda tu haki kwa mke na jamaa wengine, au kutenda tu haki kwa wale wanaofanya biashara pamoja nawe, au kuwatendea haki na kuwatendeamema viongozi wako au wale waliopo chini yako, bali kiwango cha uadilifu kilichowekwa na Mwenyezi Mungu ni kutenda haki kwa maadui zako, kwani uchaMungu wa kweli wapatikana pale ambapo adui pia hutendewa kwa haki na kwa uadilifu. Ndipo mtu atakapopata kiwango kile kinachotakiwa kipatikane kwa mwaminio wa kweli,ndipo njia za mahubiri zitafunguliwa na mafundisho ya kweli ya Islam yataeleweka kwa wengine wasiokuwa Waislamu.
Pia hapa mwishoni, Mwenyezi Mungu Anasema kwamba 'Mungu Anakiona kila kitu mnachokifanya.Ikiwa nyinyi mnakosa viwango hivi, basi hamwezi kuwa watu wenye uchaMungu.MwenyeziMungu, kwa kutumia neno qawwam, Alituamrisha tushike uadilifu siku zote.

Kuhusiana na hilo, Sayyidna Ahmad as anasema:
'Mwenyezi MunguAlisema, kuhusiana na suala la uadilifu usioweza kupatikana bila kufuata ukweli: Na uadui wa watu usiwashawishini ya kwamba msifanye uadilifu. Shikeni uadilifu,kwani ucha Mungu umo humo humo.
'Sasa mnafahamu ya kuwa mataifa yenye kufanya dhulma na maudhi na kumwaga damu na kuvamia na kuwaua watoto na wanawake kama walivyofanya makafiri wa Makka na tena wawe wakiendelea na vita,kufanya uadilifu kwa watu wa namna hiyo ni vigumu kiasi gani, lakini ndani ya Qur'an Tukufu, haki ya maadui hao pia imezingatiwa na imehamasishwawafanyiwe uadilifu,lakini wewe uliyezungushwa na ubaguzi, utayaelewaje mambo haya matakatifu?
Ingawaje imeandikwa katika Injili ya kuwa wapendeni maadui zenu, lakini haikuandikwa kuwa uadui na dhuluma ya mataifa isiwazuie nyinyi kufanya uadilifu wa kweli.Mimi nasema kwelikweli kwamba, kuwatendea maadui kwa upole ni rahisi, lakini kuzilinda haki zao na kushika uadilifu kamili katika kesi zao mbalimbali ni vigumu sana, na hii ni kazi tu ya watu wenye moyo mkubwa.

Ni wengi ambao huonesha mapenzi fulani kwa maadui zao na kuongea nao kwa upole, lakini wanawanyang'anya haki zao.Ndugu fulani anampenda nduguye na kwa kutumia njia hiyo ya kumpenda, anamdanganya na kumnyang'anya haki zake. Kwa mfano kama ni mkulima, basi kwa kutumia ujanja wake, analifuta jina lake kutoka kwenye karatasi za mirathi, na kidhahiri anaonesha kwamba anampenda sana.Basi Mwenyezi Mungu Hakueleza mapenzi haya katika aya hiyo, bali Ameeleza kiwango kinachotakiwa cha mapenzi nacho ni uadilifu.
Alisema ya kuwa atakayefanya uadilifukwa adui wakemkubwa na kutouepuka ukweli na uadilifu, basi huyo ndiye mwenye mapenzi ya kweli. Basi hiki ndicho kiwango kile ambacho tunapaswa kujitahidi kuwa nacho.
Baada ya kutimiza wajibu wetu kuhusiana na uadilifuunaoihusu jamii katika nyakati mbali mbali,amri nyingine itolewayo na Mwenyezi Mungu ni hii kwamba: timizeni ahadi ya Allah.Kuna fundisho jingine la Islam lililo bora, na amri nyingine ya Allah imeelezwa hapa ya kwamba, kutekeleza amri zote ni muhimu kwa binadamu ili aweze kuboresha uzuri wa dini na khulka zake kulingana na jinsi Mwenyezi Mungu Alivyoeleza amri mbali mbali katika Qur'an Tukufu.

Pia Alisema kwamba; hayo yote muyatekeleze kwa lengo la kupata radhi ya Allah,hapa Alisema kwamba hii inaweza kufanyika wakati ambapo mioyo yenu itakuwa safi na iwe imejaa kwa jazba hii ya kwamba kila kitendo nitakachokifanya nitafanya kwa nia ya kutimiza ahadi yangu niliyoifanya na Muumba wangu, na ahadi kubwa kabisa ambayo mwaminio huwa anafanya na Allah, na haswa ahadi ya mwanajumuiya, ni ahadi ya baiat.Ikiwa tutambue umuhimu wa ahadi hiyo basi itakuwa rahisi kutekeleza amri zote na kutenda mema.
Ahadi iliyochukuliwa na Syedna Ahmad as katika masharti ya baiat, ambamo ndani yake ametulazimisha kwa namna ambayo, tukiendelea kuyarudia mara kwa mara, basi jamii ya kiahmadiyya inaweza kuepukana na maovu yote.
Kimuhtasari naeleza hapa kwamba katika masharti ya baiat tunaahidi nini?Jambo la kwanza ndilo hili kwamba hatutamshirikisha Mungu na chochote mpaka tuingie kaburini. Na ushirikina una aina tofauti ambazo nimekwishaeleza mapema katika hotuba zangu zilizotolewa katika mwezi wa Ramadhani. Kisha kujiepusha na kusema uongo,uzinzi,ufisadi,ufidhuli,hiyana na uasi na hayo pia nimekwishayaeleza. Na hatashindwa na tamaa hizo mbaya. kisha awe anasali sala tano kila siku na kumsalia Mtume saw na kuzikumbuka hisani za Mwenyezi Mungu na kumhimidia juu ya hayo.
Wahamiaji wengi waliofika hapa kutoka Pakistan kutokana na hali ngumu ya nchi, wamefanyiwa hisani kubwa na Mwenyezi Mungu kwamba Amewapa uhuru wa kuishi na pia kuboresha hali yao ya uchumi, basi badala ya kuonesha kiburi au fahari yoyote, wanapaswa kumhimidi Mwenyezi Mungu juu ya neema Yake hii,wanapaswa kumshukuru Allah. Wasimdhuru mtu yeyote kwa namna yoyote na waridhike na kudra ya Allah bila ya kulalamika.Mwenyezi Mungu Akimneemesha, basi amshukuru juu ya hilo na akikabiliana na mtihani wowote basi asimlaumu kamwe.
Akiepukana na desturi za kidunia na kujiepusha na tamaa zote,atekeleze amri za Mwenyezi Mungu na mtume wake,kwa kuacha kiburi na majivuno,ashike unyenyekevu na kuipenda heshima ya Islam zaidi kuliko nafsi yake,mali yake na watoto wake na ajitahidi kwa uwezo wake wote kuwahurumia viumbe na kuwanufaisha binadamu, anapaswa kuwa na jadhba ya kuitumikia jamii na kisha kuonesha mfano wa hali ya juu katika kumpenda Yeye na kumtii na kutojali kitu chochote mbele ya mapenzi yake.Basi hiyo ndiyo ahadi tuliyoifanya tulipoingia ndani ya jumuiya. Kila mmoja anapaswa kuangalia kwamba ni kwa kiasi gani tunatimiza ahadi yetu.

Katika mwezi wa Ramadhani tunapata nafasi nyingi ya kutenda mema,pia tulipaswa kuangalia na inabidi tuonekuwa leo ni siku ya mwisho wa mwezi,bali tunatakiwa tuangalie, kwa mwaka mzima, ya kwamba yale ambayo tumeyafanya yawe yanaendelea kwa siku zote,kwamba ni kwa kiasi gani tunayatekeleza,kwa kiasi gani tunatimiza ahadi yetu tuliyoifanya na Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu Anasema endapo mtaahidi hivi, mtapata malipo makubwa,malipo ambayo hamwezi kuyafikiria,mkiahidi basi muitimize ahadi hiyo,kisha Mwenyezi Mungu pia Anasema kwamba mtakapotimiza ahadi yenu, basi Mwenyezi Mungu, kwa kuisafisha mioyo yenu na kuitakasa na uchafu wote, Atawaingizenindani ya wachaMungu ambao watakuwa wapendwa wake,ambao Mwenyezi Mungu Anawapenda. Msidhani kuwa msipotimiza ahadi yenu basi hamtapata malipo mema, bali mjue kwamba mtaulizwa kuhusu ahadi yenu,katika hizo ahadi za aina zote zimo ambazo zimefanywa na Allah Taala na watu wake.
Kwa mfano katika hotuba yangu iliyopita kumbukumbu kuhusu malezi ya mayatima imepita.kuchukua dhima ya kuwalea mayatima pia ni ahadi mbele ya Allah, msipoutekeleza wajibu wenu huo, basi mtakuwa mnavunja ahadi ambayo mtaulizwa na Allah Taala,vivyo hivyo kama kuna viongozi wasiotekeleza majukumu yao ya utawala, nao pia wataulizwa na kama hawatimizi haki ya raia, pia wataulizwa.Kwa bahati mbaya katika nchi za Kiislamu viongozi wote wana hali hiyo hiyo. Hawatekelezi wajibu wao wala hawatoi haki za wanadamu wenzao, na wamekaa bila ya hofu, kana kwamba hawataulizwa, Allah Taalah Anasema, kwa yakini wataulizwa.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Answarullah Waweka Kambi ya Tarbiyyat Masjid Salaam

Na Mwandishi wetu
Dar es Salaam

Mnamo siku ya Jumamosi na Jumapili ya tarehe 12 na 13 ya mwezi Oktoba, 2013 Majlis Answarullah Ilaqa ya Dar es salaam, iliandaa kambi ya Tarbiyyat kwa wanachama wake. Kambi hiyo ilikuwa ndani ya Masjid Salaam na Answarullah takriban 60 hivi walihudhuria.

Kambi ya Tarbiyyat iliendeshwa chini ya uwenyekiti wa Bwana Abedi Iddi ambaye ni Nazim wa Ilaqa ya Dar es salaam. Kiongozi mkuu wa Tanzim nchini Tanzania, Muadhamu Sadri Sahib Inayatullah S. Nakuchima alifunguwa rasmi kambi hii.

Katika khutuba yake ya ufunguzi, Sadr Sahib alirejea maneno ya Huzur (atba) aliyokuwa ametamka mwaka 2003 katika Jalsa Salana ya kule Uingereza. Katika Khutuba hiyo Khalifa Mtukufu alisema "Katika shughuli zozote za kidini ni muhimu sana kukaa na kusikiliza kwa makini na kuhakikisha kuwa masomo yote mliyojifunza mnayafatiliya kwa makini sana. Kama hamtafanya hivyo, basi mtalingana na wale watu waliosemwa na Kurani Tukufu kuwa ukiwaonya au usiwaonye hawatabadilika. Ni viziwe, mabubu na juu ya macho yao kuna kifuniko na kwa hiyo hawaoni chochote. Na katika hali kama hiyo hata asimame mcha Mungu wa hali ya j uu namna gani kwenu kutakuwa hakuna manufaa yoyote yale. Lakini kama mkikaa na kusikiliza kwa makini masomo yote kisha mkayafanyia kazi masomo hayo, basi akisimama mcha Mungu wa hali ya chini sana na akawakumbusheni wajibu wenu na mkayatekeleza, kwa hakika mtanufaika sana na masomo hayo yote"

Ndipo Sadr sahib akakaziya kuwaambia Answarullah waliohudhuria na kushiriki kwenye kambi hii kuwa makini sana na masomo yote yatakayoletwa kwao, si hivyo tu, bali watakaporudi matawini mwao wafatilie kila walichojifunza kwenye kambi hii. Kambi ilianza kupokea mada mbalimbali kutoka kwa wahusika. Mada ya kwanza Ansarullah waliyoelezwa ilikuwa kuhusu mahusiano bora ya ndoa maudhui yake ilitolewa na Mwalimu Abdulrahman Ame. Mudri wa mapenzi ya Mungu na piya ndiye katibu wa malezi wa Jamaat, Muadhamu Mahmood Hamsini Mubiru alizungumzia juu ya tukio la kihistoria. Bwana Ramzan Fazal ambaye ni Naib Sadr alitowa mada juu ya umuhimu wa kusimamisha swala. Mukarramu Bwana Mussa Mpinga aliwakilisha mada ya Tabligh shirikishi ambayo wana kambi nao walishiriki kutowa maelezo yao.

Baada ya swalatul Fafri kulikuwapo darasa. Darasa liliendeshwa na Mwalimu Hassan Mwalimu Sakulo ambaye alizungumzia juu ya Wasiya wa Hadhrat Luqman kwa mwanaye ambamo ndani yake tunapata somo zito. Kwenye kambi hii, Ustadh Mwalimu Abdullah Mbanga alielezea mada kuhusu wajibu wetu mkubwa tulionao juu ya Kurani Tukufu. Mzee Hemedi Sheikh Ubwa alizungumzia nidhamu ya kukopeshana ndnai mkiwamo uaminifu. Baada ya hapo kipindi cha maswali mchanganyiko kikawasili. Maswali yalijibiwa na Mwalimu Abdurahman Ame, Bwana Ramzan Fazal na Ustadh Mwalimu Abdullah Mbanga.

Baada ya kipindi hicho, Katibu wa Tabligh kitaifa, Bwana Ally Khamisi Mbambwa ambaye pia alikuwa mratibu wa kambi hii ya Tarbiyyat, aliwakilisha mada juu ya umuhimu wa kujitolea katika njia ya Allah. Aliyekhitimisha kwa waleta mada alikuwa Bwana salumu Dadi Mtamila ambaye alizungumzia mada kuhusu Mtume Muhammad (saw) ni rehema kwa ulimwengu. Kambi hii ya Tarbiyyat ilifungwa na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jamaat Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Mbashiri Mkuu aliwaambia Answarullah kuwa watende kazi zao sawasawa na miongozo inayotolewa na Tanzim yao. Alitaka shughuli za Tabligh zisisinzie hata kidogo na alitaka kila Answarullah ashiriki katika hilo bila kukosa. Alisema kwamba wengi kati yetu tumepatikana kwa njia ya Tabligh, kwa hiyo upo umuhimu wa kuwaita wengine katika mtindo huo huo.

Sheikh alisema pia kwamba Tajnid ni muhimu mno. Alisema kwamba Mwezi Julai mwaka huu alipokwenda kule Uingereza kwa ajili ya Jalsa Salana, aliulizwa na Khalifa Mtukufu Answarullah idadi yao ni wangapi katika Tanzania. Kwa hiyo Sheikh akasema kwa kuhimiza, Tanzim ihakikishe inakuwa na Tajnid halisi ya wanachama wake.

Jambo jingine ambalo Sheikh alizungumzia ni juu ya kuowa na kolewa nje ya Jumuiyya. Alitowa agizo zito kabisa kwa Tanzim kuanzia sasa ni marufuku Answarullah kuowa nje ya Jamaat. Bali agizo



Bw. Inayatullah Seif Sadr Ansarullah Sahib akisisitiza jambo wakati wa Kambi ya Tarbiyyat

hili ni kwa kila Ahmadiyya, aliowe wala mwanamke wa Kiahmadiyya siolewe na mtu ambaye si Mwana Jamaat. Ndoa zisimame kwa Wanajumuiyya tu bila kuchanganya na wa kule. Wale ambao hadi sasa wanaishi na mke au na waume wasiokuwa Wanajumuiyya, basi wafanye nao mazungumzo kwa upole na hekima, huenda Allah Akawaokoa, lakini kama haiwezekani basi Mwanajumuiyya atazame na aheshimu zaidi dini yake.

Kadhalika Mbashiri Mkuu alihimiza kila Answarullah awe na mawasiliano ya MTA ili kupata khabari na maagizo mbalimbali kutoka kwa Khalifa Mtukkufu. Aliwataka wale wenye TV, lakini hawana dishi, ni vizuri sasa wajitahidi kupata dishi. Kama kutakua na ugumu Fulani wowote kupatikana hilo dishi na vifaa vinginevyo ni vyema Ofisi yake ikaelezwa ili kuona inaweza kusaidia namna gani katika hilo.

Kwa ujumla tuseme kambi hii ya Tarbiyyat si kwamba watu walichota tu elimu na maarifa, bali kwa kweli ilikuwa kambi ya kuwaongezea Answarullah imani na kuwasogeza kuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu. Kwa sababu, kwa pamoja Answarullah hao walikuwa wanamsabihi Subhana Wataala na walishiriki kwa pamoja vile vile kwenye ibada ya swala za kawaida na tahajjudi. Kwa hakika ilikuwa kambi ya malezi.

Mwenyezi Mungu Atubariki na Atuwezeshe kuyafanyia kazi haya yote. Amin.

YA RABI TUNAKUOMBA

1 Bismillahi Rabana,
ndiye Allah Mwenyezi
Ndiwe wewe Maulana,
ndiye Mola Laazizi
Twakushukuru kwa kina,
tumepata mazowezi
Ya Rabi tunakuomba,
tuwe karibu na Wewe

2 Ni tangia pale jana,
hadi leo twabarizi
Siku mbili hizi Bwana,
tumepatiwa ujuzi
Mengi tumeelezana,
ya nyendo na simulizi
Ya Rabi tunakuomba,
tuwe karibu na Wewe

3 Ladha tuliyoiona,
kwenye siku mbili hizi
Mfano wake hakuna,
wallahi nasema wazi
Mioyo ilivyonona!,
vipi ingekuwa mwezi?
Ya Rabi tunakuomba,
tuwe karibu na Wewe

4 Mema tumeusiana,
nuru ikidawirizi
Swala usiku mchana,
kiswali bila ajizi
Ni kambi iliyokuna,
imeleta mageuzi
Ya Rabi tunakuomba,
tuwe karibu na Wewe

5 Kambi yetu Subhana,
imezidisha mapenzi
Mapenzi ya kupendana,
bila ya upatilizi
Hapa tulivyoshibana,
kama mmoja mzazi
Ya Rabi tunakuomba,
tuwe karibu na Wewe

6 Japo leo twaachana,
tumepata andalizi
Ingawa tutaagana,
bado kwako waombezi
Utamu tumeuona,
kukuacha hatuwezi
Ya Rabi tunakuomba,
tuwe karibu na Wewe

7 Na Wewe tutashikana,
kwenye mema maongozi
Yale yatayotubana,
katika yetu makazi
Wakumuomba hatuna,
ila Wewe Mtanguzi
Ya Rabi tunakuomba,
tuwe karibu na Wewe

8 Muhammad Sayidina,
swalallahu mwangalizi
Sisimko la aina,
yanimwagika machozi
Ya Rabul alamina,
kambi yetu ya malezi
Ya Rabi tunakuomba,
tuwe karibu na Wewe

Ni shairi ambalo lilisomwa na Bwana Ally Khamisi Mbambwa, siku ya mwisho ya kambi ya Tarbiyyat ya Answarullah ya Ilaaqa ya Dar es salaam. (Mudri).

Je wajua habari hizi?

Na Mwandishi wetu

Tanzim ya Majlis Answarullah Tanzania chini ya uongozi wa Sadr sahib Muadhamu Inayatullah S. Nakuchima, imeanzisha shamba la mihogo. Shamba hilo lipo kule Kitonga kwenye eneo la Jamaat. Shamba linaendeshwa kwa njia ya Wakar Amal. Yaani kila wiki Wana Answarullah hujitolea siku ya Jumamosi na Jumapili kwenda kushughulikia shamba hilo. Shamba limeleta manufaa kidogo. Mwaka huu shamba hilo limetowa neema kwa shule yetu ya Kitonga. Sadri sahib alikabishi mihogo iliyozalishwa kwenye shamba hili kwa Mwalimu Mkuu wa shule yetu ya Kitonga. Katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani wanafunzi wetu walipata futari kutoka shamba hili.

Mwaka huu, mnamo mwezi wa Oktoba, 2013 shughuli za shamba hili kwa kuliendeleza zimeanza. Qaid Dhahanat Wasihat Jisman, Bwana Abdullah Mikendo anawataka Answarullah wote wa Ilaqa ya Dar es salaam kujitokeza kila pale wanapotakiwa kufika kwenye shamba hili kwa njia ya Wakala Amal. Mwaka huu linapanuliwa.

Pia Answarullah wote wanakumbushwa kila m moja awe na baiskeli. Yaani kila mmoja wetu awe anamiliki chombo hiki na kukitumia ili mwili upate msukumo wa kupata siha n jema. Taarifa inatakiwa imfikie Sadri sahib nani amekamilisha jambo hili. Baadhi ya Answarullah wa Ilaqa ya Dar es salaam wameuahidi uongozi kwamba mpaka mwishoni mwa mwezi Desemba m waka huu watakuwa wameshanunua baiskeli hizo, Inshallah. Lakini ninyi je, wa huko vipi? Tuleteeni taarifa.

Wakati huo huo, uongozi wa Answarullah Ilaqa ya Dar es salaam umeanzisha utaratibu naweza kusema mzuri wa kuwapatia elimu wanachama wake. Umepanga pawe na masomo mara nne kwa wiki. Jumatatu hadi Alhamisi nayo yatafanyika jioni baada ya swalatul Asri hadi saa 11:30. Darasa hili ni la masomo matatu; Kujifunza usomaji wa Kuarni Tukufu, kujifunza Lugha ya Kiarabu na kujifunza Fiq'hi. Masomo haya yameshaanza tarehe 21/10/2013 ndani ya Masjid Salaam. Darasa lina waalimu watatu pia, Mwalimu Hamidii Juma Kaigwa kutoka Kitonga secondary, Naib Sadr I Bwana Abdullah Nasoro wakiongozwa na Ustaadhi Mwalimu Abdullah Mbanga. Answarullah wote wal Ilaqa ya Dar es salaam wanatakiwa kushiriki katika darasa hili ambalo watu watajipatia elimu. Je, unafahamu elimu haina mwisho? Fika Darasani sasa.

MWAKA MPYA WA TAHRIK JADID 2013/2014

Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry anapenda kuwatangazia Wanajumuiya wote kwamba Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) ametangaza mwaka mpya wa Tahrik Jadid kwa kipindi cha 2013/2014.

Kufuatia tangazo hilo kila kiongozi wa familia anawajibika kutoa ahadi za wanajumuiya wote walio kwenye familia yake bila kusahau watoto wachanga.

Kwa muongozo kutoka Markaz Majlis Amila Taifa imepitisha kuwa mwaka huu kuwe na orodha ya watoto maalum ambao wazazi wao watawaahidia kiasi cha Tsh 10,000/- (elfu kumi) au zaidi. Kiwango hiki ni hiyari na sio lazima. Mtoto atakayeahidiwa chini ya kiwango hicho hataingia kwenye orodha hiyo maalum.

Wanajumuiya ambao hawakukamilisha ahadi zao za mwaka uliopita wanatakiwa kukamilisha ahadi zao hizo sambamba na kutoa na kulipia ahadi za mwaka mpya.

Taarifa za ahadi kutoka kila tawi zinatakiwa ziwasilishwe mapema Makao Makuu. Mwisho wa kuwasilisha ni tarehe 31 Disemba 2013.

Pia Taarifa zinaweza kutumwa kwa njia ya mtandao. Kwa maelezo zaidi mnaweza kuwasiliana na Amiri K. Abedi, Katibu Taifa Tahrik Jadid 0655199997 au 0754967720 au amirabeid@yahoo.co.uk

IJTIMAA YA ANSARULLAH INAKARIBIA

Tumo kwenye mwezi Novemba sasa, mwezi ujao ni Desemba. Mwezi Desemba katikati, yaani tarehe 14 na 15, 2013, Tanzim ya Majlis Answarullah Tanzania kama kawaida itafanya Ijtimaa na shura. Shughuli hizi zitateendeka kule Kitonga Inshallah. Siku zimekaribia mno, tuwe tayari kuhudhuria Ijtimaa hii bila kukosa. Sadri sahib, muadham Inayatullah S. Nakuchima anategemea kwamba kila Answarullah ametimiza wajibu wake wa kutoa michango yake yote na sasa anasubiri muda tu wa kufika kwenye viwanja vya shughuli zetu.

Wajumbe wote wa Ijtimaa na shura wanategemewa kuwapo kwenye viwanja na ukumbi wa mikutano yetu kule Kitonga kuanzia tarehe 13 Desemba 2013, Mwenyezi Mungu Amfikishe hapa kila mjumbe salama usalimini.

Pamoja na hayo, Sadri sahib anamkaribisha kila mtu anayependa kusikia, kuona na kushuhudia ukweli wa Seyidna Ahmad (as) wale walio karibu na pale tunapofanyia shughuli zetu tunawakaribisha sana.

Tafadhali karibuni nyote.

Maana ya kweli ya Jihadi Katika Uislamu

Kutoka uk. 10

Masihi Aliyeahidiwa a.s. na Muslih Maud, alivyofafanua juu ya hili kwenye kitabu chake cha Hakika ya Ahmadiyya.

Ameandika:

Kosa jingine lililoenea ni shauri la jihadi. Wako watu wanaosema ya kwamba Waahmadiyya wanaikataa jihadi. Lakini sivyo. Waahmadiyya hawaikatai jihadi. Waahmadiyya. Wanayoyasema ni haya; vita vinakuwa namna mbili. Vita mojani ya jihadi, na vita nyingine ni vita tu. Vita ya jihadi ni vita inayopiganwa kwa sababu ya kulinda dini, na kushindana na maadui wanaotaka kufuta au kuingamiza dini kwa upanga, na wanataka kuibadilisha imani ya watu kwa ncha ya jambia. Kama matukio ya namna hii yatukie katika dunia, basi vita vya jihadi vinakuwa lazima juu ya kila Mwislamu. Lakini ina sharti moja ya kuwa tangazo la jihadi ya namna hii litangazwe na Imamu (mkubwa na kiongozi wa umma) ili Waislamu wajue nani anatakiwa kuingia katika jihadi hii na nani wanatakiwa kungoja zamu yao. Kama haitakuwa namna hii, basi kila Mwislamu atayeingia katika jihad atakuwa na dhambi. Lakini kama itatangazwa na Imamu, Mwislamu atakayekuwa na dhambi ni yule ambaye anaitwa lakini hahudhurii katika jihad. Waahmadiyya walipokuwa wanaikataa vita ya jihadi walikuwa wakikataa kwa sababu Waingereza hawakuwa wenye bidii ya kubadilisha dini za watu kwa nguvu ya upanga. .. (Hakika ya Ahmadiyya uk. 12 - 13).

Pia Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad r.a. amesema:

Kama ambavyo sala ni faradhi, vile vile haja inapozuka, kupigana kwa ajili ya imani ni faradhi. Yapaswa ikumbukwe kwamba katika mambo ambayo yametajwa kuwa ni misingi ya imani moja wapo ni Jihadi … Yule nayeikimbia Jihadi pale inapokuwa ni faradhi anahukumiwa kuingia motoni. (Report of the Majlis Mushawarat, 1950)

Hivyo basi wale wanaosambaza uongo kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. amekataza au amefuta jihadi wanafanya hivyo ama kwa chuki tu au kwa uelewa wao mbovu wa Jihadi.

Lakini ni nani mwenye akili zake na mchunguzi makini anayeweza kuthubutu kusema kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. amekataza jihadi wakati ambapo Waahamdiyya wanajitolea mali zao na nafsi zao kila siku kwa ajili ya dini ya Mweneyzi Mungu.

Ni nani anayeweza kusema kwa hoja ya akili kwamba maelfu ya wabashiri na waalimu wa Kiahamdiyya duniani kote, waliojitolea waqfu maisha yao , wakiwacha ndugu na jamaa zao, kwa ajili ya dini ya Mweneyzi Mungu tu, kwamba hao hawafanyi jihadi au kwamba hawajaelewa maana ya kweli ya jihadi.

Hivyo wasikilizaji wapendwa, naomba nimalizie hotuba yangu kwa kuyanukuu tena maneno ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. niliyokwisha kuyanukuu huko mwanzoni:

Amesema:

Nimekuja kwenu na amri: Jihadi kwa panga kuanzia wakati huu na kuendelea imekwisha, Jihadi ya kuzitakasa roho zenu lazima iendelee. Sisemi haya kwa utashi wangu. Kwa hakika huu ni utashi wa Mungu.

Jihadi ya siku hizi ni kulieneza neno la Islam, kujibu hoja za wapinzani, kutangaza sifa za dini ya Islam na kutangaza ukweli wa Mtume Mtukufu s.a.w. ulimwenguni kote. Hii ndio Jihadi inayotakiwa mpaka MM atakapobadilisha hali ya dunia.

Mwisho

Wasifu wa mzee Ramadhani Abdallah

Na Mzee Jumanne Rajabu - Morogoro

Usiku wa tarehe 27/07/2013 Wanajumuiyya wa Morogoro Mjini walipokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa sana taarifa ya kifo cha ghafla cha Mwanajumuiyya Mkongwe wa Tawi la Chamwino Morogoro Mjini marehemu Ramadhani Abdallah.

Tarehe 05/07/2013 marehemu Mzee Ramadhani Abdallah alihudhuria sala ya Ijumaa katika Masjid Nasrat Morogoro Mjini. Maskini Mzee Ramadhani bila kujijua kuwa sala ile ya Ijumaa ilikuwa sala yake ya mwisho ndani ya Masjid Nasrat. Marehemu Mzee Ramadhani alikuwa akiugua maradhi ya pumu (Asthma) kwa kipindi kirefu. Hakika sisi wote ni wa Mwenyezi Mungu na bila shaka kwake tutarejea.

Marehemu Mzee Ramadhani Abdallah alizaliwa mwaka 1936 mkoani Morogoro, na alijiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya mnamo miaka ya 1960. Marehemu ameacha Mjane na watoto wa kike wawili (2) kati ya watoto wake 11. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahala pema peponi, Amin.

Madhumuni na lengo na shabaha ya kila Mwanajumuiyya ni kuishi maisha ya hapa



Mzee Ramadhani Abdallah akiwa kwenye Jalsa 2011

duniani sawa na masharti ya Baiat. Marehemu Ramadhani Abdallah alijitahidi kwa upande wake kupata shabaha ya lengo hilo, na kushikilia katika njia ya Islamu. Wakati wa uhai wake Mzee Ramadhani ilikuwa ni jambo la nadara sana au hata pengine ilikuwa ni jambo lisilowezekana kumkosa Mzee Ramadhani katika sala ya siku ya Ijumaa, kinyume chake sababu itakuwa ugonjwa au safari. Marehemu Mzee Ramadhani alikuwa mtu mpole msikivu na mwenye tabasamu na mchangamfu na mcheshi wakati wote. Hata itakumbukwa katika Jalsa ya mwaka 2012 ambayo ilikuwa ndiyo Jalsa yake ya mwisho kuhudhuria marehemu Mzee Ramadhani alipata fursa ya kutoa historia fupi ya jinsi alivyojiunga na Jamaat na matukio yaliyomkuta mara baada ya kujiunga.

Itakumbukwa katika dakika hizo chache alizopewa kuelezea historia yake, ukumbi mzima uliridhima kwa vicheko na nderemo zilizoambatana na Takbira nyingi kuashiria furaha na msisimko wa jazba uliochochewa na simulizi tamu iliyojaa kila aina ya vionjo kutoka kwa Marehemu Mzee Ramadhani Abdallah.

Nidhamu yake Marehemu kwa viongozi wake wa dini na Wanajumuiyya wenzie ilikuwa ya hali ya juu sana. Marehemu Mzee Ramadhani alikuwa mstari wa mbele katika kutoa michango yake ya Jumuiyya, katika kazi za Waqar Amal (kazi za kujitolea), pamoja na Tabligh, licha ya umri wake kuwa mkubwa. Pia katika uhai wake marehemu Ramadhani Abdallah aliwahi kushika nyadhifa mbalimbali katika Majlis Amila ya tawi la Morogoro Mjini.

Marehemu Ramadhani Abdallah amezikwa katika kijiji chake cha Lugala Mkoani Morogoro 28/07/2013 kwa taratibu na nidhamu ya Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Tunamuomba Allah amkubalie mja wake huyu kwa jitihada zake na amsamehe madhaifu yake na makosa yake na ampe mapumziko kwenye pepo yake ya milele. Amin.

Maana ya kweli ya Jihadi Katika Uislamu

Kutoka uk. 11

walioleta maana potofu ya Jihadi. Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

Baadhi ya Waislamu wagomvi na wajinga huuita umwagaji damu wa kikatili kuwa jihadi na hawatambui kwamba kumpinga mtawala mwadilifu ni uasi na sio Jihadi. Zaidi ya hayo mtu anayevunja ahadi anayefanya uovu badala ya kufanya tendo jema na anayewatweza wasio na nguvu ni mdhalimu na sio shujaa wa vita. Tohfah Qaisariyyah in Ruhani Khaza'in, vol. 12, p.280.

Akieleza madhara ya uelewa huo potofu wa jihadi Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

"Itikadi ya Jihadi kama ilivyoeleweka na inavyoenezwa na viongozi wa Kiislamu wa zama hizi wanaoitwa maulvi ni potofu kabisa"

"Haitapelekea chochote isipokuwa kwa kuhubiri kwao huko watawabadilisha watu wa kawaida kuwa wanyama wa porini na watawafanya waondokewe na sifa zote nzuri za kibinadamu na haya ndiyo yaliyotokea.

Mimi natambua kwa hakika kwamba mzigo wa dhambi za wale wanaofanya mauaji kwa ujinga kwa kufuata mahubiri kama haya, na ambao hawajui sababu gani Islam ililazimika kupigana vita katika siku zake za mwanzo uko katika shingo za hawa maulvi ambao wanaendelea kueneza kwa siri itikadi hizi hatari ambazo matokeo yake ni kupotea kwa uhai kunakosikitisha"

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anaendelea kusema:

"Kwa hakika mtazamo huu wa jihadi unaipa Islamu sura isiyopendeza kabisa na kwa kuleta uadui na chuki miongoni mwa wasio waislamu, huwatenga mbali na Islam kwa namna isiyoweza kufutika. Kila mtu atatetemeka kwa hofu anapokutana na Muislamu aliyepotoka kama hivyo, kwa manaa wakati wowote anaweza kuchagua kuwa Ghazi wa kumfanyia kazi ya mkato. Jambo hili kwa hakika litakwaza lengo lenyewe hasa la Islam, ambalo ni kuwapata wanadamu wote kwa kuhubiri ujumbe wake wa upendo na amani.

Hakuna ukweli hata chembe katika kauli ya kwamba huu ni wakati wa kushika panga na bunduki ili kueneza dini ya kweli na ucha Mungu. Panga, mbali kabisa na kuonyesha uzuri na ubora wa ukweli huufanya uonekane wa hovyo na kuuficha nyuma. Wale wanaoshikilia mawazo kama hayo si marafiki wa Islam bali ni maadui wake wa hatari sana. Wao ni wenye nia mbaya, wenye asili chafu, roho hafifu, mawazo finyu, akili zilizodumaa na muono mfupi. Wao ndio wanafungua mlango wa kukataliwa kwa Islam - . kukataliwa ambako uhalali wake hauwezi kuhojiwa.

Wanasema kwamba Islam inahitaji panga kwa maendeleo yake, kwa njia hii wanaupaka matope usafi wake na kutia kiwingu katika jina lake tukufu. Dini ambayo inaweza kiurahisi kuthibitisha ukweli wake na ubora wake juu ya zingine kwa hoja nzito za kielimu, haihitaji upanga kuwatisha watu na kuwalazimisha kukubaliwa nao kwa nguvu. Dini inastahili kuitwa dini pale tu inapokuwa inaendana na akili. Ikishindwa kutimiza kigezo hiki, ikiwa inabidika kujazia upungufu wake wa hoja kwa kushika panga basi haihitaji hoja nyingine kuthibitisha kwamba ni dini ya uongo. Upanga ulioishika unakata kwanza shingo lake yenyewe kabla ya kuwafikia wengine.

Akionesha kwamba islam haihitaji vita kwa ajili ya kukubalika kwake Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

Hakuna mwislamu yeyote wa kweli ambaye amewahi kuamini ya kwamba Islam inapaswa kuenezwa kwa upanga. Islam siku zote imekuwa ikienezwa kwa sifa zake yenyewe. Wale ambao kwa kujiita waislamu wanataka kuieneza islam kwa upanga hawana habari ya sifa zake nzuri na hivyo mwenendo wao unafanna na na mwenendo wa wanyama wa porini. (Tiryaqul Qulub Now printed in Ruhani Khazain (London, 1984), Vol. 15, p. 3 5, footnote) .

Akiwaelekea wafuasi wake kuwaongoza kwenye jihadi ya kweli Masihi Aliyeahidiwa a.s. anawahimiza:

Katika wakati huu kimahususi naielekeza Jumuiya yangu wanaonikubali kuwa ni Masihi Aliyeahidiwa, kwamba daima wakae mbali na tabia hizi chafu. Mungu amenituma kuwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na amenivika vazi la Masihi a.s. Mwana wa Mariamu.

Kwa hiyo ninawausieni; epukaneni na uovu na muwe na huruma ya kweli kwa wanadamu. Safisheni nyoyo zenu dhidi ya chuki na kinyongo, kwa maana kwa kushika tabia hii mtakuja kuwa kama malaika. Ni chafu na haifai dini ile ambayo inakosa huruma kwa wanadamu, na imechafuka njia ile iliyojaa kisirani kwa msingi wa tamaa za kibinafsi … kuweni na huruma kwa wote kwa ajili ya Mungu ili kwamba muweze kuonyeshwa ukarimu kutoka mbinguni. Njooni na nitakufundisheni njia ambayo itafanya nuru yenu ing'ae juu ya nuru zote. Acheni bughudha zote na uovu na wahurumieni watu na jitupeni kwa Mungu ...

.. Nimekuja kwenu na amri: Jihadi kwa panga kuanzia wakati huu na kuendelea imekwisha, Jihadi ya kuzitakasa roho zenu lazima iendelee. Sisemi haya kwa utashi wangu. Kwa hakika huu ni utashi wa Mungu.

Tafakarini hadithi iliyomo katika Bukhari ambamo imesemwa kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. ataondosha kupigana kwa ajili ya imani. Sawa na hilo ninawaamuru wale waliojiunga na kundi langu kwamba waziache fikra kama hizo. Wazitakase nyoyo zao na kukuza ukarimu wao na wanapaswa wawahurumie wenye shida. Waeneze amani duniani kwa kuwa kwa kufanya hivyo wataifanya dini yao ienee.

Pia Masihi Aliyeahidiwa a.s. anazidi kusema:

Jihadi ya siku hizi ni kulieneza neno la Islam, kujibu hoja za wapinzani, kutangaza sifa za dini ya Islam na kutangaza ukweli wa Mtume Mtukufu s.a.w. ulimwenguni kote. Hii ndio Jihadi inayotakiwa mpaka Mwenyezi Mungu atakapoibadilisha hali ya dunia. (Letter addressed to Mir Nasir Nawab Sahib).

Wasikilizaji wapendwa,

Nadhani sitokuwa nimeitendea haki mada hii iwapo sitogusia japo kidogo juu ya ile hoja ya wale waislamu wanaotangaza kimakosa kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. amefuta jihadi, na kwamba aliwalaza usingizi mnono waislamu wa India wasipigane jihadi dhidi ya serikali ya kiingereza kwa vile alikuwa ni kibaraka wa wa serikali hiyo.

Katika kujibu hoja hii, hatuna budi turudi nyuma kidogo tuangalie hali ilivyokuwa wakati wa ujio wa Masihi Aliyeahidiwa a.s..

Itakumbukwa kwamba kabla ya ujio wa utawala wa Kiingereza huko India, sehemu kubwa ya Punjab ilitawaliwa na Masingasinga ambapo utawala wao ulikuwa wa udhalimu mkubwa dhidi ya Waislamu.

Akiwakumbusha Waislamu jambo hili Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

Waislamu bado hawajasahau wakati ambao katika mikono ya Masingasinga walihukumiwa kutupwa kwenye jiko linalowaka moto na sio tu kwamba dunia yao ilikuwa imeanguka bali dini yao pia ilikuwa katika hali mbaya zaidi. Ilikuwa ni vigumu kwao kutimiza wajibu wao wa kidini, kiasi hiki kwamba katika tukio moja Mwislamu aliuwawa kwa kutoa adhana tu. (Announcement of 10 July 1900).

Utawala huu wa kidhalimu wa Masingasinga umeelezewa pia kwenye vitabu vingi vya historia:

Katika (Encyclopedia of Sikh Literature, p.1127), imeandikwa:

Ilionekana kwamba Masingasinga walikuwa na chuki kubwa dhidi ya Waislamu. Waislamu wanaume, wanawake na watoto waliuwawa bila huruma, vijiji vyao vilibomolewa na kubakishwa magofu, wanawake wao walidhalilishwa na maelfu ya misikiti ilibomolewa.

Katika hali kama hiyo, utawala wa Kiingereza ukaja nchini India na kwa kadiri kubwa ukaleta hali iliyo bora sana kwa waislamu na watu wote wa India. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akilikumbusha jambo hili anasema:

Baada ya utawala wa Kiiengereza kushika mahala pa utawala wa Masingasinga, katika upande huu wa nchi mkutano ulifanyika huko Allahbad mnamo Novemba 1, 1858, ambapo ilitangazwa kwa niaba ya Malikia Victoria kwamba:

"Tunatangaza kuwa ni matakwa na furaha ya ufalme wetu kwamba hakuna yeyote kati ya wananchi wetu ambaye atanyimwa haki au kupendelewa kwa msingi wa imani ya dini yake, wala kwa msingi huo mtu hatanyimwa usalama wake. Mbele ya macho ya sheria watu wote watakuwa na haki sawa ya kulindwa.

Serikali inawapa watu wote uhuru kamili wa kueneza dini zao na kwa njia hii watu wanapatiwa nafasi ya kusoma na kutafakari juu ya misingi ya kila dini… hii ndio sababu sisi katika maandiko yetu na hotuba zetu huwa tunataja wema wa serikali ya Uingereza (Roedad Jalsa Dua).

Ni kwa sababu hii ya uhuru wa kuabudu na uadilifu wa serikali ya Kiingereza ndipo Masihi Aliyeahidiwa a.s. akaandika mengi ya kuisifia serikali hiyo, ambapo ni mambo hayo ndiyo yanayonukuliwa kimakosa kwa makusudi na waislamu katika kupotosha ukweli. Hata hivyo kama maandishi haya ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. yasomwe kwa makini yataonesha bayana kwamba alichokuwa anakifanya sio kusifia tu bali hasa ni kuondoa uelewa mbaya juu ya Islam na kueleza uzuri wake kwa lengo la kumhubiri Malkia na watendaji wa serikali yake.

Kwa mfano katika kitabu chake cha Tohfai Qaisariyyah; zawadi kwa Malkia, Masihi Aliyeahidiwa a.s. akieleza misingi ambayo ametumwa kwayo anasema:

Na kanuni ya pili ambayo nimeimarishwa juu yake ni kusahihisha maana isiyo sawa ya jihadi inayojulikana baina ya baadhi ya Waislamu wasio na elimu. Mwenyezi Mungu Amenifahamisha kwamba zile njia zinazofahamika siku hizi kuwa jihadi ni kinyume kabisa na mafundisho ya Kurani Tukufu. Hakuna shaka kuwa ndani ya Kurani Tukufu mlikuwa na agizo la kupigana vita ambalo lilikuwa lielewekalo zaidi akilini na lenye kupendeza zaidi kuliko lile la vita vya Yoshua mwana wa Nuni. Na sababu yake ilikuwa tu kwamba wale walioziinua panga bila ya haki kwa ajili ya kuwaua Waislamu na kumwaga damu bila ya haki na kufikisha dhuluma kwenye upeo wa mwisho, hao tu ndio wauawe kwa panga. Lakini hata hivyo adhabu hii haikuwa kali sana kama vita vya Musa, bali yule mtu aliyeomba hifadhi – kwa kusilimu kama yu Mwarabu, au kwa kutoa jizia kama si Mwarabu – basi adhabu hiyo ilikuwa haitolewi.

Ilmuradi, katika zama za Mtume wetu s.a.w sababu hasa ya jihadi ya Kiislamu ilikuwa hii hii kwamba ghadhabu ya Mwenyezi Mungu iliwaangukia waliokuwa wakifanya dhuluma. Lakini kuishi chini ya kivuli cha uadilifu wa serikali adilifu - kama ulivyo utawala wa Malkia wetu muadhamu, Malkia wa India halafu kukusudia kuiasi siyo jihadi, bali hilo ni wazo lililojaa unyama na ujahili wa hali ya juu kabisa. Ile serikali ambayo ndiyo sababu ya kuishi maisha ya uhuru na kupata amani kikamilifu na kuweza kutekeleza faradhi za kidini barabara, kuwa na nia mbaya dhidi yake na kuitekeleza ni harakati yenye hatia na siyo jihadi. Ndiyo sababu Mungu Hakukipenda kitendo cha wale wenye kuleta uhaini mnamo mwaka 1857, na hatimaye wakakumbwa na aina mbali mbali za adhabu kwa sababu walipambana na serikali yao mhisani na mlezi.

Basi, Mwenyezi Mugu Ameniimarisha katika msingi huu kwamba serikali mhisani kama ilivyo serikali hii ya Uingereza, itiiwe kikweli na ishukuriwe kikweli. Hivyo, mimi na Jumuiya yangu tumeshikamana na kanuni hii. Nami kwa kulitekeleza suala hili nimeandika vitabu vingi sana kwa Kiarabu, Kiajemi na Kiurdu na humo nimeandika kinaga ubaga namna Waislamu wa India ya Uingereza wanavyoishi kwa utulivu chini ya serikali hii ya Kiingereza na namna wanavyoweza kuhubiri dini yao kwa uhuru, na wanatekeleza faradhi zao zote bila ya kizuizi. Halafu hata kuwaza tu moyoni kufanya jihadi dhidi ya serikali hii yenye baraka na yenye kutoa amani ni dhuluma na uasi sana namna gani. (zawadi kwa Kaisari uk. 15 - 18).

Pia naomba nimnukuu Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad, Khalifa wa Pili wa

Endelea uk. 9

Maana ya kweli ya Jihadi Katika Uislamu

Kutoka uk. 12

Uislamu wenyewe, waislamu na wanadamu kwa ujumla.

Hivyo kufahamu maana sahihi ya jihadi ni jambo linalolihitajika mno na kila binadamu aliyeko juu ya uso wa ardhi leo ima awe mwislamu au la.

Hivyo mada yangu hii itaangazia kwa muhtsari maana ya kweli ya jihadi, sawa na mtazamo wa mtukufu Mtume s.a.w. / au sawa na mafundisho sahihi ya Islam.

Jihadi ni neno la Kiarabu ambalo linatokana na mzizi wa ***jahada*** likiwa na maana ya kujitahidi mno, kwa umakini mkubwa na kwa kudumu, bila kuchoka wala kukata tamaa katika kufikia lengo fulani. Hivyo katika istilahi ya Kiislam, Jihadi ni kujitahidi kwa kudumu, kwa umakini mkubwa na bila kuchoka wala kukata tamaa kuhakikisha kwamba mtu anayafuata mafundisho ya Mwenyezi Mungu ipasavyo.

Kwa mujibu wa Kurani Tukufu na Hadithi za mtukufu Mtume s.a.w. Jihadi imegawanyika katika makundi au madaraja matatu makubwa:

Kuna:

i. Jihadi ndogo
ii. Jihadi kubwa
iii. Jihadi kuu (au jihadi kubwa kabisa).

Tukianza na hii ya tatu yaani Jihadi kuu au jihadi kubwa kabisa, hiyo ni jitihada ya mtu kupambana na nafsi yake mwenyewe dhidi ya vishawishi vya shetani ambavyo daima vinamvuta aachane na mafundisho ya Mwenyezi Mungu. Hii huitwa jihadi kuu kwa sababu humtaka mtu apambane dhidi ya nia mbaya za nafsi yake, dhidi ya utashi wake, dhidi ya matamanio yake, dhidi ya dhamira yake isiyoonekana kwa dhahiri na hivyo kupambana nayo kunahitaji, maamuzi, umakini na uthabiti wa nia wa hali ya juu - na kwa hakika jambo hilo ni gumu sana na wakati huo huo ndio msingi wa kila hatua ya kujitakasa - yaani kuacha maovu na kutenda mema.

Hii hasa ndio maana ya aya zile nilizozisoma mwanzoni.

Katika aya zote hizo jihadi imeambatanishwa na: Kuwa na imani thabiti juu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kufanya juhudi katika kazi za kuimarisha dini ya Mwenyezi Mungu, kutenda mema, kutoa mali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kujitolea nafsi (yaani kuifanya nafsi yako kuwa si chochote mbele ya heshima ya dini ya Mweneyzi Mungu.

Jihadi ya pili (ya daraja la Pili - jihadi kubwa) ni juhudi ya kuitangaza dini ya Mwenyezi Mungu kwa wasio Waislamu (kufanya tabligh) pamoja na kujibu hoja na shutuma zote za wapinzani wa dini ya Mwenyezi Mungu. Tena jihadi hii lazima ifanywe sio kwa mawazo binafsi ya mtu bali kwa kutumia muongozo wa Kurani Tukufu. Jihadi hii inaitwa jihadi kubwa kwani nayo inahitaji maamuzi ya dhati pamoja na mtu kujitolea mali yake na nafsi yake kwa kudumu.

Kuhusu aina hii ya jihadi Mwenyezi Mungu anasema:

Basi usiwatii makafiri na ushindane nao kwa (Qur'an) hii mashindano makubwa (jihadi kubwa). 25:53.

Jihadi ya aina ya tatu au tuseme ya daraja la tatu ambayo huitwa jihadi ndogo ndiyo ile ambayo wengi wanaielewa kuwa jihadi ya pekee nayo ni kupambana kwa silaha na adui aliyeamua kuwadhulumu Waislamu na kuwazuia wasitekeleze dini yao. Hii imeitwa jihadi ndogo na Mtukufu Mtume s.a.w. kwani ni aina ya jihadi yenye masharti, Ni jihadi ambayo hailazimiki kufanywa hadi pale kunapokuwa na mazingira yanayolazimisha kufanyika kwake.

Moja kati ya sharti za lazima za kupigana jihadi ya vita ni hili kwamba Waislamu ni lazima wawe wamefanyiwa dhuluma kwanza kwa kuuwawa na kuzuiwa kwa nguvu wasimwabudu Mola wao.

Mwenyezi Mungu anasema:
Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa; na kwa yakini Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kuwasaidia.
Waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu wanasema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu. 22:40-41.

Wakati fulani Mtukufu Mtume s.a.w. na maswahaba zake waliporudi kutoka kwenye kupigana vita, alisema: *Raja'naa minaljihadil asghar ilal jihadil akbar* - Tunarejea kutoka kwenye jihadi ndogo kuelekea kwenye jihadi kuu. Yaani kutoka kwenye jihadi ya kupambana na adui kwa silaha na kuelekea kwenye jihadi ya kupambana na nafsi zetu wenyewe. Ndio kutokea kwenye jihadi ndogo kuelekea kwenye jihadi kuu kabisa.

Pia Mtukufu Mtume s.a.w. anaripotiwa kusema: 'Mbora wa wapiganaji jihadi ni yule anayepambana na nafsi yake.'

Jihadi ya vita imeitwa jihadi ndogo kwa sababu sio ya kudumu na iwapo hali hiyo (ya kudhulumiwa kiasi hicho) haipo, basi jihadi hii pia haipo, wakati ambapo aina zingine za jihadi ni za kudumu daima na hakuna muda ambao kunakuwa na sababu ya kutokufanyika kwake.

Hizi ndizo maana sahihi za jihadi na yeyote anayeleta au mwenye mawazo kinyume na haya huyo hajaelewa chochote katika Islam.

Wasikilizaji wapendwa,

Sasa nitaingia katika kujibu shutuma za wale wasio Waislamu dhidi ya maana hii iliyo bora ya Jihadi, na pia nitaelezea upotofu wa tafsiri ile mbovu inayotolewa na baadhi ya waislamu. Hata hivyo yanibidi nikiri kwamba mimi mwenyewe sina uwezo wala siwezi kuwa na maneno ya kuwajibu watu hao, bali kazi hiyo mahsusi alipewa Masihi wa zama - mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Hivyo basi nitanukuu kutoka maandishi yake na semi zake kuhusu jambo hili.

Akijibu hoja iliyoletwa na mtu mmoja asiye Muislamu ambaye alitoa tafsiri mbovu ya jihadi, Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliandika:

"Mpinzani huyu ametaja jihadi inayopatikana katika Islam na anafikiria kwamba Quran inaamuru vita hii takatifu bila vigezo. Hakuwezi kuwapo uzushi mkubwa zaidi ya huo. Quran inaruhusu tu kupigana na wale wanaowazuia watu wa Mungu kuamini na kuingia katika dini yake na kushika amri za Mungu na kumwabudu Yeye. Na Mungu anaruhusu kupigana dhidi ya wale wanaowashambulia Waislamu pasi na haki wanaowatoa waaminio majumbani mwao na katika ardhi zao, na kuwalazimisha waja wa Mwenyezi Mungu kufuata dini yao kwa nguvu, na wanaotaka kuiangamiza dini ya Islam na kuwazuilia watu kujiunga na Islam na kuwa Waislamu. Nurul-Haqq, part 1 in Ruhani Khaza'in, vol. 8, p.62.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

Inatakiwa pia ikumbukwe kwamba Islam inaruhusu kushika panga dhidi ya watu ambao wenyewe wanakuwa wa kwanza kushika panga, na inaruhusu kuwauwa wale ambao wenyewe wamekuwa wa kwanza kuua. Haielekezi kwamba Waislamu wawapo chini ya mtawala ambaye si mwislamu ambaye anawatendea kwa haki na usawa, washike silaha dhidi yake kwa uasi. Kwa mujibu wa Qura'ni Tukufu hii ni njia ya wakosefu na sio ya wachamungu. (Anjam Aatham, p. 37).

Kuhusu wale waislamu

Endelea uk. 10

Tishio la Kuzuka Vita ya Tatu ya Dunia

Kutoka uk. 12

hali ya wasiwasi imelikumba taifa lote la Syria na kwamba hakuma sehemu ya nchi hiyo iliyo salama. Aidha, alionyesha wasiwasi wake kwamba makundi ya kigaidi na yale yenye msimamo mkali yaliyopo nchini humo na nje ya nchi hiyo yameungana na majeshi ya upinzani ya waasi wa Syria. Amesema, huku makundi hayo yakiwa yanadai kuwasaidia wananchi wa Syria lakini ukweli ni kwamba wanajali tu maslahi yao binafsi na uharibifu watakaousababisha kwenye nchi hiyo utaendelea kwa muda mrefu.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) amesema kwamba sababu ya msingi wa machafuko katika baadhi ya nchi za Kiislamu ni kwamba siku hizi Serikali za Kiislamu zimekwenda mbali kabisa na mafundisho ya msingi ya Islam.

Khalifa Mtukufu amesema:

"Qurani Tukufu imewataja Waislam kama 'umma uliobora' lakini ni lipi jema lifanywalo na viongozi wa Kiislam katika ulimwengu wa leo? Hawana chembe yoyote ya huruma wala mapenzi na hawafuati mafundisho ya kweli ya Islam. Hawana heshima na uadilifu na wanatafuta msaada kutoka kwa wafadhili wan je ili tu waendelee kuwaua ndugu zao."

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) kisha alieleza msingi wa kurejesha amani ya Syria kwa kuzingatia mafundisho ya Q'urani Tukufu. Amesema Q'urani Tukufu inaeleza bayana kuwa pindi pande mbili zinapohitilafiana ni jukumu la majirani zao kujitahidi kutafuta ufumbuzi kwa njia ya mazungumzo ya amani kwa kuzingatia usawa na uadilifu. Amesema Q'urani Tukufu imeweka wazi kwamba uadui au chuki miongoni mwa mataifa usiwafanye mkaachana na uadilifu. Suluhu na amani lazima viendelee kuwa ndio jambo muhimu kuliko kulipa kisasi au kuendeleza maslahi binafsi au ya taifa fulani.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliendelea kusema kwamba ulimwengu wa Kiislam ungepaswa kuchukua jukumu la kutatua mgogoro wa Syria.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) amesema:

"Umoja unaowakilisha nchi za Kiislam 'Organization of Islamic Countries-OIC' ulitakiwa tangu mwanzo kabisa kuchukua jukumu la kuendeleza amani nchini Syria kwa kuzingatia kwamba wote wanamwabudu Mungu Mmoja, wanamfuata Mtume yuleyule na wanakiamini Kitabu Kitukufu. Nchi za kiislam zilitakiwa kukutana na kutafuta amani kwa kuzingatia mwongozo sahihi uliotolewa na Q'urani Tukufu."

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) amesema kwamba mara kwa mara amekuwa akiwakumbusha viongozi wa dunia na wanasiasa kuhusiana na suala muhimu linalohitajika kwa sasa ambalo si lingine bali ni suala la amani kwa kuzingatia uadilifu wa kweli. Khalifa Mtukufu (a.b.t.a) amesema kwamba Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya kwa kutumia raslimali chache ilizonazo imeeneza ujumbe huu wa amani katika sehemu kubwa ya dunia. Ameshauri kwamba waahmadiyya wanatakiwa waendeleze juhudi hizi za kueneza ujumbe wa amani huku wakimwomba Mwenyezi Mungu aiokoe dunia dhidi ya maangamio.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) amesema:

"Waislam Ahmadiyya kote duniani lazima waombe amani na kuiombea dunia iokolewe dhidi ya kila aina ya maangamio na majanga. Lazima tuombe kwa sababu bwana wetu, Mtukufu Mtume Muhammad (S.a.w) alikuja kwa ajili tu ya kuanzisha fungamano la mapenzi kati ya mja na Muumba Wake na kueneza amani duniani."

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) amesema sio kazi ya Serikali za kigeni kutoka nje kujihusisha moja kwa moja na migogoro hii. Aliongeza kuwa hata katika hatua hii inayoonyesha kuchelewa na kukata tama, Serikali za Kiislam zinatakiwa zitekeleze wajibu wao huu.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) amesema:

"Hata sasa Serikali za Kiislam zinatakiwa kuonyesha hali ya heshima na uadilifu. Badala ya kuangalia maslahi yao binafsi wanatakiwa watoe kipaumbele kwa ajili ya maslahi na ustawi wa ulimwengu wa kiislam. Hili linawezekana endapo tu hofu ya kweli ya Mwenyezi Mungu itajengeka katika nyoyo za watawala wa Serikali na raia, na linawezekana endapo tu watafuata mfano mwema wa Mtukufu Mtume Muhammad (S.a.w)."

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alihitimisha kwa kuombea amani ya dunia na pia kumwomba Mwenyezi Mungu ajaalie (makundi ya kiislam yanayofarakana) yaelewe na kutekeleza wajibu wao.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

DhulQa'dah/Hijja1434AH | Sept./Okt. 2013 | Ikha/Tabook 1392HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Usamah r.a ya kwamba Mtume s.a.w. alipita kikao cha watu ambamo walikuwemo Waislamu, Washirikina, wenye kuyaabudu masanamu n wayahudi. Mtume s.a.w. aliwatolea salamu. (*Bukhari*)

Tishio la Kuzuka Vita ya Tatu ya Dunia

• *Kiongozi wa Waislamu Duniani Aonya*

Na Jamil Mwanga, Dar es Salaam

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya Duniani, Khalifa Mtukufu Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (Mwenyezi Mungu Amsaidie) ametaka kuwepo kwa uvumilivu dhidi ya Syria na kutaka usawa na uadilifu utawale katika kushughulikia mgogoro huo.

Kiongozi huyo ambaye ni Khalifa wa Tano wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya ameonyesha wasiwasi wake kuhusiana na athari itakayotokea baada ya kuivamia Syria kijeshi.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) amesema kwamba uvamizi huo utasababisha mgogoro wa Syria kuenea zaidi na hatimaye kusababisha kuzuka kwa Vita ya Tatu ya Dunia. Amesema njia pekee ya kutatua mgogoro huu ni ni kuendelea kutenda kwa kufuata mafundisho ya Q'urani Tukufu ya kushikamana na haki na usawa.



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.ba, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya Duniani

Akizungumzia kuhusiana na hatari zilizotokana na mgogoro wa Syria, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) amesema tayari mgogoro huo umesababisha mgawanyiko na mfarakano duniani. Amesema wakati baadhi ya nchi zenye nguvu zikiungana na Serikali ya Syria, nchi nyingine zenye nguvu zinaunga mkono majeshi ya waasi wa Serikali ya nchi hiyo. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) amesema mgawanyiko huu **"umesababisha hali ya mambo kuwa tete."**

Akizungumzia kuhusiana na athari za mgawanyiko huu, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) amesema:

"Endapo nchi zenye nguvu zitajihusisha moja kwa moja na nchini Syria itasababisha madhara sio tu kwa nchi za kiarabu bali pia kwa mataifa mengine. Inaonekana kwamba mataifa mengi yenye nguvu hayatambui kwamba vita hivyo havitabakia Syria pekee, bali ni dalili bayana ya Vita ya Tatu ya Dunia."

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) amesema ni jambo la kusikitisha kwamba mgogoro wa Syria umesababishwa na Waislam, ambao wote wanadai kufuata imani ya Kiislam (Kalima). Amesema vita na

Endelea uk. 11

Maana ya kweli ya Jihadi Katika Uislamu

Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa salana 2013

Na Mwl. Abdulrahman M. Ame - Dar es Salaam

Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia Zetu. Na bila shaka Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wafanyao mema. 29:70

Enyi mlioamini! je, Niwajulisheni biashara itakayowaokoeni katika adhabu iumizayo? Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na jitahidini katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu; hayo ni bora kwenu ikiwa mnajua. 61:11-12.

Kama aya hizi zinavyoonesha, Jihadi ni moja kati ya mafundisho mazuri na ya msingi ya Islam. Mwislamu hawezi kufikia kuwa Muumini wa kweli kama hajafanya jihadi. Hata hivyo fundisho hili ni miongoni mwa mafundisho ya Islam yaliyoeleweka vibaya sana, kuchafuliwa na kupotoshwa kabisa.

Kwa wengi wasio Waislamu, inapotajwa jihadi, picha inayojengeka machoni pao ni ya mtu mwenye kanzu chafu na ndevu ndefu akiwa na macho ya kutisha kwa ghadhabu alizonazo, huku mkononi mwake akiwa ameshika upanga (au siku hizi bunduki, mabomu na hata mzinga), tayari kumfyeka na kumuondolea mbali yeyote asiye mwislamu.

Ufahamu huu mbaya wa wasio Waislamu kwa kadiri kubwa unachangiwa na baadhi ya Waislamu wenyewe, ambapo wako wengi wanaoamini na kuhubiri kwamba: Muislamu wa kweli ni yule ambaye muda wote yuko tayari kutumia silaha kupambana na asiye Mwislamu hadi pale atakapoamua kusilimu - na kwamba hiyo ndiyo jihadi. Pia wako wadhaniao kwamba haifai kwa Muislamu kuridhia kuishi chini ya utawala wa mfalme asiye mwislamu na kwamba ni kupambana na utawala usio wa kiislamu mpaka pale utakapoanguka na mahala pake kushikwa na waislamu ili waweze kutekeleza 'sharia' - na kwamba hiyo ndiyo jihadi.



Mwl. Abdulrahman M. Ame, akitoa hotuba kwenye Jalsa Salana 2013

Kwa kufuata uelewa huu usio sahihi, baadhi ya Waislamu wanamtoa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na Jumuiya yake nje ya Islam kwa madai kwamba eti amefuta jihadi na kuwakataza Waislamu wasipigane jihadi dhidi ya serikali. Kwa mfano kule India ilisemwa kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni kibaraka wa Waingereza kwa kuwa nasaha zake ziliwataka waislamu wasipigane na serikali ya Kiingereza.

Kutokana na uelewa huu mbovu, uzuri wote na umuhimu wote wa Jihadi umepotea na kugeuzwa kichwa chini miguu juu na badala ya jihadi kutoa matunda yake mema na matamu yaliyokusudiwa, uelewa huu umezaa matunda machungu yaliyoudhuru mno

Endelea uk. 11